

**ATHARI YA UTENZI KATIKA UANDISHI WA RIWAYA TEULE YA
KISWAHILI.**

NA:

JUDITH KHASOA NABANGI

C50/CE/27925/2013

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI
KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA
CHUO KIKUU CHA KENYATTA.**

JUNI, 2017

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu na haijawahi kuwasilishwa popote na yeyote kwa minajili ya shahada yoyote.

JUDITH KHASOA NABANGI

C50/CE/27925/2013.

(MTAHINIWA)

TAREHE

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu:

DKT. EDWIN MASINDE

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

TAREHE

DKT. TITUS KAU

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

TAREHE

IKISIRI

Utafiti huu umejikita katika kuonyesha athari ya utenzi katika uandishi wa riwaya teule ya Kiswahili. Matumizi ya utenzi katika uandishi wa riwaya ni mojawapo ya mbinu za kimtindo za uandishi. Kwa hivyo, utafiti huu umefanywa kwa kuongozwa na malengo matatu ambayo ni: Kudhirisha jinsi utenzi umechangia uandishi wa riwaya kimaudhui. Pili, kuonyesha mtindo ulivyochangiwa na utenzi katika kuandika riwaya teule. Tatu, kubainisha jinsi wahusika wa riwaya teule wamechangiwa na utenzi. Utafiti ulifanywa ili kuonyesha usemezano wa utenzi na riwaya teule ya Kiswahili. Utafiti huu ulifuata muundo wa kimaelezo na ulifanyiwa maktabani. Utafiti uliongozwa na nadharia ya usemezo ya Mikhail Bakhtin, ambayo inashikilia kwamba tanzu za fasihi husemezana. Sampuli lengwa katika utafiti huu ilikuwa riwaya tatu ambazo ziliteuliwa kimaksudi; *Kasri ya Mwinyi Fuad, Msimu wa Vipepeo na Walenisi*. Data ilikusanywa kwa kusoma riwaya hizo tatu kwa kina na kunukuu mambo muhimu yanayohusiana na utafiti huu. Mambo haya ni maudhui, mtindo wa uandishi wa riwaya na wahusika wa riwaya teule. Data hiyo ilichanganuliwa kwa kuzingatia maswali ya utafiti. Utenzi unawiana vipi na uandishi wa riwaya kimaudhui? Pili, utenzi unawiana vipi na riwaya teule kimtindo? Tatu, je, kuna uwiano upi baina ya wahusika wa utenzi na wale wa riwaya teule? Aidha, data ilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti, pia, iliongozwa na mihimili ya nadharia ya usemezo. Matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa kwa njia ya maelezo na utoaji wa mifano mwafaka. Utafiti huu uligundua kwamba athari za utenzi katika uandishi wa riwaya ni mojawapo ya mbinu za kimtindo za uandishi. Kwa hivyo, kipengele cha utanzu mmoja kinaweza kutumiwa kama mbinu ya kimtindo katika uandishi wa utanzu mwingine.

ABSTRACT

An epic is a genre of literature which has contributed in the writing of the Swahili novel. This research seeks to establish how an epic has influenced the writing of a novel. This research was guided by the following objectives: First, to show that the themes found in an epic are the same ones found in the novel. Secondly, to show how an epic can be used as a style in the writing of a novel. Thirdly, to explain the comparison between the characters of an epic and those ones found in the novel. This research was done in the library. Mikhail Bakhtin's theory of dialogism was used. The research was based on the principle which asserts that all the genres of literature 'dialogue'. The research sample was purposefully selected where three novels were chosen. The novels include: *Kasri ya Mwinyi Fuad*, *Msimu wa Vipepeo* and *Walenisi*. Data was collected through indepth reading of the selected novels. The data was then analysed basing on the research questions and objectives. The analysis was also based on the tenets of the theory. The research findings were given out through explanations and quoting of relevant examples from the selected novels. It was found that an epic as a genre of literature can be used as a style in the writing of a novel.

TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu wapendwa marehemu mzee John Nabangi Were pamoja na mama Grace Nakhumicha Nabangi kwa kuniwekea msingi bora wa masomo.

Kwa mume wangu, Andrew Mbere Wafubwa, ulinitia moyo wakati mambo yalikuwa magumu kimasomo. Ulinihimiza kila mara nisome. Asante kwa kunipa mazingira mema yaliyoniwezesha kukamilisha kazi hii.

Kwa watoto wangu, Sharleen Nandako, Bradley Nabangi na Bryton Barasa, mlivumilia mengi nilipokuwa masomoni. Nawashukuru kwa kunihimiza kila mara nitie bidii.

SHUKRANI

Namshukuru mola wangu kwa kunipa nguvu na siha njema ili kuiendeleza kazi hii. Jina lako na litukuke ulimwenguni kote. Pia, shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Edwin Masinde na Dkt. Titus Kaui kwa kunielekeza wakati wote nilipokuwa nashughulikia kazi hii. Nimepata maarifa mengi kuhusiana na utafiti.

Shukrani kwa wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili kwa msaada na motisha walionipa kwa masomo haya. Asante sana Dkt. Richard Wafula kwa kunimakinisha kuhusu nadharia ya Usemezo na jinsi ya kuitumia katika utafiti huu.

Shukrani pia zimwendee mume wangu na watoto wangu waliostahimili kutokuwepo kwangu wakati wote nilioshughulikia masomo yangu. Ufanisi huu ni wetu sote.

Asanteni sana wazazi wangu kwa malezi yenu mema na kwa kuipanda mbegu ya masomo maishani mwangu. Nashukuru ndugu yangu na dada zangu wote kwa kunitia ari ya kuendelea mpaka nikamaliza masomo yangu hususan dada Ruth Kiluyi Wakapisi kwa kunihimiza nisichoke hasa mambo yalipokuwa mazito kwangu.

Shukrani zangu pia ziwaendee walimu ambao pia ni wanafunzi wenzangu walionitangulia hasa Joseph Mulalu, George Kasili na Charles Omutimba kwa kuisoma na kuifanyia marekebisho tasnifu hii tangu mwanzo wake hadi tamati. Natambua mchango wa kila mmoja hata kama sikukutaja, neema za Mungu ziwe juu yenu.

UFAFANUZI WA DHANA

Bahari	Ni kina cha mshororo wa mwisho wa kila ubeti wa utenzi.
Jagina	Shujaa
Kani pewa	Huu ni muhimili wa nadharia ya usemezano ambao hutenganisha maandishi au masimulizi.
Kani kitovu	Huu ni muhimili wa nadharia ya usemezano ambao huleta mshikamano katika maandishi au masimulizi.
Kanivali	Ni sherehe ya kitamaduni kule Ulaya ambapo watu hujivisha maguo na mafigu yanayozisitiri sura zao na kufanya mambo ya kiucheshi na sarakasi.
Kronotopu	Ina maana ya mabadiliko ya maana ya maneno kwa kurejelea mpito wa wakati.
Masimulizi ya sira	Masimulizi kuhusu mtu yanayojitokeza kama wasifu au tawasifu
Matini	Kazi ya kifasihi. Ni kifungu cha maandishi au lugha.
Mtagusano	Mvutano katika mawasiliano au katika nafsi.
Mwingilianomatini	Ni uzalishaji wa maana ndani ya matini na wala siyo ndani ya mahusiano ya matini mbalimbali.
Sajili	Mitindo ya matumizi ya lugha ambayo hutumika katika hali tofauti za kijamii.

Sira	Masimulizi ambayo ni ya kweli kuhusu habari za maisha ya mtu
Usemezo	Hii ni nadharia inayohusishwa na Mikhail Bakhtin ambaye anaitumia kuelezea uhusiano unaokuweco katika mawasiliano. Yaani ni mtagusano unaohusu zaidi ya nafsi mbili unaohusu mvutano katika mawasiliano.
Usemi	Maneno yanayozungumzwa.
Utenzi	Ni kisa au hadithi ndefu ya kihistoria inayohusu shujaa wa kike au wa kiume aliyewahi kuishi au anayeaminika kuishi.

YALIYOMO

UNGAMO.....	ii
IKISIRI.....	iii
ABSTRACT.....	iv
TABARUKU.....	v
SHUKRANI.....	vi
UFAFANUZI WA DHANA	vii
YALIYOMO.....	ix
SURA YA KWANZA	1
1.1 Usuli wa Mada.....	1
1.1 Suala la Utafiti	4
1.2 Maswali ya Utafiti.....	5
1.3 Madhumuni ya Utafiti.....	5
1.4 Sababu za Kuchagua Mada.....	5
1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....	6
1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada.....	7
1.6.1 Kuhusu Maudhui.....	7
1.6.2 Kuhusu Mtindo	8
1.6.3 Kuhusu Wahusika	10
1.6.4 Kuhusu Nadharia	11
1.7 Msingi wa Nadharia.....	13
1.8 MBINU ZA UTAFITI	19
1.8.0 Muundo wa Utafiti.....	19
1.8.1 Mahali pa Utafiti	20
1.8.2 Uteuzi wa Sampuli.....	20
1.8.3 Njia ya Ukusanyaji Data	21

1.8.4 Uchanganuzi wa Data	21
1.8.5 Uwasilishaji wa Matokeo.....	21
1.9 Kiishilio	22
SURA YA PILI.....	23
2.0 Athari Ya Maudhui Ya Utenzi Katika Riwaya Teule	23
2.1 Utanguliizi	23
2.2. Historia na Maendeleo ya Utenzi na Riwaya ya Utenzi na Riwaya.....	23
2.3 Maudhui ya Utenzi Katika Riwaya Teule.....	25
2.3.1 Dini Katika Riwaya Teule.....	26
2.3.2 Malezi Katika Riwaya Teule.....	31
2.3.3 Ndoa Katika Riwaya Teule.....	34
2.4 Kiishilio	36
SURA YA TATU.....	37
3.0 Athari ya Mtindo wa Utenzi Katika Riwaya Teule.....	37
3.1 Utangulizi.....	37
3.2 Usimulizi Katika Riwaya Teule.....	38
3.3. Uunganifu Katika Riwaya Teule	41
3.4 Matumizi ya Lugha	45
3.4.1 Taswira.....	45
3.5 Kiishilio	48
SURA YA NNE	49
4.0 Athari ya Wahusika Majagina wa Utenzi Katika Riwaya Teule	49
4.1 Utangulizi.....	49
4.2 Taathira ya Wahusika Majagina wa Utenzi Katika Riwaya Teule	49
4.3 Kiishilio	58
SURA YA TANO	59

5.0 Muhtasari na Matokeo ya Utafiti	59
5.1. Utangulizi.....	59
5.2 Muhtasari	59
5.3 Matokeo ya Utafiti	61
5.4 Changamoto	69
5.5. Mapendekezo	69
Marejeleo	71
KIAMBATISHO A	76
Utenzi wa Mwana Kupona.....	76
KIAMBATISHO B	93
Utenzi wa Fumo Liyongo	93

SURA YA KWANZA

1.1 Usuli wa Mada

Tangu kuumbwa kwa mwanadamu, lugha ndicho kipawa anachokitumia ili kuelezea hisi zake, tajriba za maisha na fikra alizonazo bongoni mwake (Bakhtin,1981). Mwanadamu ameweza kuelezea matukio muhimu katika maisha yake kiutunzi. Miongoni mwa tungo hizo ni utenzi na riwaya, ambazo ni tanzu za fasihi.

Fasihi hutumia lugha kwa ufasaha kama malighafi na kuumba kazi kama vile hadithi, riwaya, tamthilia, ushairi au utenzi. Njogu na Chimera (1999) wakimnukuu Roman Jakobson wanaeleza kwamba, fasihi ni matumizi ya nguvu dhidi ya lugha ya kawaida kimaksudi. Aidha, wanaeleza kwamba lugha inayotumiwa katika kazi ya fasihi inapendeza, inavutia na kutamanisha kuitafakari maradufu. Mawazo haya yanatiliwa nguvu na mawazo ya wanamuundo wa Kirusi Victor Shklovsky na Boris Tomashevsky wanaosema kwamba fasihi ni matumizi maalum ya lugha.

Utafiti huu umelenga kuonyesha namna sifa za utenzi zinavyojitokeza katika uandishi wa riwaya teule. Hii ikiwa ni mojawapo ya mbinu za kimtindo za uandishi wa riwaya. Utafiti umechunguza namna utenzi unavyosemezana kimaandishi na riwaya teule.

Finnegan (1970), anafafanua utenzi kama shairi refu lenye beti nyingi ambazo zina mizani chache au mishororo mifupi ambayo kwa asili haina vina vya kati. Utenzi kwa kawaida huwa na maudhui ya kidini, vita, ushujaa, tukio la kizamani au la kihistoria. Vutagwa (2013), anaeleza kuwa utenzi ni kisa au hadithi ndefu ya kihistoria inayohusu shujaa wa kike au wa kiume aliyewahi kuishi au anayeaminika aliishi. Aghalabu tenzi hugawika katika mistari minne. Anaongeza kusema kwamba, tenzi ni nyingi hasa katika

jamii za Uswahilini. Baadhi ya tenzi ni kama vile; *Utenzi wa Howani, Mwana wa Howani, Mwana kupona, Mwana Fatuma, Al Inkshafi, Ukombozi Wa Kenya, Ukombozi wa Zanzibar, Utenzi wa Fumo Liyongo* na nyingine nyingi.

Njogu na Chimera (1999), wanasema kuwa utenzi ni ushairi wenye mizani chache kuliko kumi na miwili, na mishororo ambayo mara nyingi haina vina vya kati katika mishororo, bali kila ubeti una vina vya namna moja katika mistari yake, isipokuwa mstari wa mwisho katika kila ubeti. Kina cha mshororo wa mwisho kinachorudiwarudiwa huitwa bahari. Tenzi nyingi husimulia visa virefu vya kihistoria, hadithi au mawaidha marefu.

Utenzi kwa mujibu wa utafiti huu ni masimulizi yanayotolewa kwa njia ya ushairi. Shairi hili lina mizani chache na hubeba maudhui ya kijamii kama vile dini, ndoa, ushujaa na historia ya jamii mbalimbali.

Mtindo wa uandishi wa baadhi ya tenzi huelekea kufanana hata kama maudhui hayafanani. Kwa mujibu wa Masinde (2003), mwanzoni mwa tenzi aghalabu mtunzi huanza kwa maombi akimshukuru Mungu, baadaye anawaomba Mtume Muhamed na maswaibu wake ili apate baraka kutoka kwa mwenyezi Mungu. Baada ya maombi, mtunzi hutunga utenzi wake, na kuelekea mwishoni mwa utunzi, mtunzi hujitambulisha jina lake na mahali anapotoka. Wahusika wa utenzi hujitokeza kikamilifu. Mhusika mkuu anaweza kuwa jagina au la. Utafiti huu umezingatia sifa za utenzi ambazo zimejitokeza kwenye riwaya teule, Sifa hizi za Kiaristotle ni kuwa utenzi una;

1. Muundo wa beti.
2. Ni utungo mrefu wenye uwezo wa kuwasilisha dhamira na maudhui ya mtunzi.

3. Uwiano au uunganifu wa visa au hadithi kimantiki katika mtiririko wa matukio.
4. Maudhui hurejelea maisha na matendo ya kishujaa kwa mfano, kuzaliwa, masaibu, dini, safari, uongozi na kifo cha shujaa anayerejelewa.

Mulokozi (1989) kwa upande mwingine anaeleza kuwa utenzi ni ushairi wa matendo. Kwa mujibu wa Mulokozi, inaonekana kwamba kuna ukaribu mkubwa kati ya utenzi na tanzu nyingine za fasihi riwaya ikiwemo. Utafiti huu umeongozwa na muhtasari wa mtazamo wa Mulokozi (2002), aliyesema kuwa utenzi una sifa zifuatazo;

- i) Ni masimulizi.
- ii) Hutolewa kishairi.
- iii) Huhusu matukio muhimu ya kihistoria na ya kijamii yenye uunganifu.
- iv) Huwasilishwa kwa kughanwa (au kuimbwa) pamoja na ala za muziki.
- v) Huelezea habari za ushujaa na mashujaa.
- vi) Hutawaliwa na muktadha wa utungaji na uwasilishaji wake kwa jamii hasa maswala ya dini, ndoa malezi na uongozi.

Kulingana na Masinde (2003), sifa hizi za Kiaristotle na Mulokozi zilikuwa dhahiri katika kipindi cha urasimi. Hata hivyo utafiti uliegemea sana sifa zilizoainishwa na Mulokozi. Baadhi ya sifa hizi za utenzi ndizo zimeingizwa katika utunzi wa riwaya ya Kiswahili. Utafiti huu umethibitisha kuwa kuna sifa za utenzi ambazo zimejitokeza katika riwaya ya Kiswahili kimaudhui, kimtindo na kwa kurejelea wahusika; huu ukiwa ndio usemezo baina ya tanzu hizi za fasihi ya Kiswahili.

Wamitila (2003), anafafanua riwaya kama kazi ya kinathari au kibunilizi ambayo huwa na urefu wa kutosha, msuko uliojengeka vizuri, wahusika wengi walioendelezwa kwa kina, yenye kuchukua muda mwingi katika maandalizi na kuhusisha mandhari maalum. Naye Bakhtin (1981), anasema kuwa riwaya ni utanzu bora kuliko tanzu nyingine za kifasihi. Utafiti huu unafafanua riwaya kama mtungo wa kinathari ambao ni mrefu, una wahusika wengi waliojengeka vizuri na huwasilisha ujumbe unaoihusu jamii ya mtunzi.

Kutokana na ufasiri huu wa dhana ya utenzi na ya riwaya, vipengele vifuatavyo vimekuwa nguzo ya kupimia sifa za utenzi katika uandishi wa riwaya teule; Matumizi ya ya lugha sanifu na msamiati wa kunata, wahusika wanaojitokeza kikamilifu, na maudhui yanayozingatiwa ni yale yanayooana na jamii husika. Utafiti huu umechunguza riwaya tatu teule ambazo ni; *Kasri ya Mwinyi Fuad, Walenisi na Msimu Wa Vipepeo*.

Utafiti umebainisha kuwa vipengele vya utanzu mmoja vinaweza kutumiwa katika kuendeleza utanzu mwingine. Ilisadifu kwamba utafiti ufanywe kuonyesha sifa za utenzi katika utunzi wa riwaya teule. Hivyo, kazi hii imeweza kutoa mchango katika usomi wa fasihi ya Kiswahili, hususa, mbinu za utunzi wa riwaya ya Kiswahili.

1.1 Suala la Utafiti

Utafiti huu umechunguza sifa za utenzi katika uandishi wa riwaya teule ya Kiswahili, hii ikiwa ni mojawapo ya mbinu za kimitindo katika uandishi wa kazi za kifasihi. Kuna mitindo mingi ambayo huweza kutumika katika uandishi wa riwaya ya Kiswahili. Utafiti huu umeonyesha kuwa kazi za kifasihi husemezana. Hii ina maana kwamba, katika kushughulikia utanzu mmoja wa fasihi, mwandishi anaweza kutumia utanzu mwingine ili kuendeleza ujumbe wake. Kwa njia hii, ilikuwa muhimu kuchunguza namna sifa za utenzi zinavyochangia uandishi wa riwaya teule ya Kiswahili.

1.2 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo;

- i) Utenzi umeathiri vipi uandishi wa riwaya teule kimaudhui?
- ii) Utenzi umeathiri vipi uandishi wa riwaya teule kimtindo?
- iii) Je, kuna athari gani baina ya wahusika majagina wa utenzi na wale wa riwaya?

1.3 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa:

- i) Kubainisha maudhui ya utenzi yalivyoathiri uandishi wa riwaya teule.
- ii) Kuonyesha mtindo wa uandishi wa utenzi ulivyoathiri uandishi wa riwaya teule.
- iii) Kubainisha wahusika majagina wa utenzi walivyoathiri wahusika wa riwaya teule.

1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Watunzi wengi wa riwaya za Kiswahili wametumia mbinu ya utenzi katika kuandika riwaya zao. Mathalani, *Msimu wa Vipepeo* na *Dharau Ya Ini* (Kyallo Wamitila), *Kisa Cha Mrina Asali* (Mathias Mnyampala), *Kasri ya Mwinyi Fuadi* (Adam Shafi Adam), na *Walenisi* (Katama Mkangi), miongoni mwa wengine wengi. Kwa hivyo sababu za kuichagua mada hii ni kama zifuatazo;

Utafiti huu ulifanywa kwa kuzingatia kwamba mbinu ya utenzi katika utunzi wa riwaya haijashughulikiwa. Hivyo utafiti ni wenye umuhimu. Pia, utafiti huu ulifanywa kwa kuzingatia kwamba kusemezana kwa kazi za fasihi kunazidi kuwa changamano zaidi. Uchangamano huu unatatiza upokeaji na uelewekaji wa maudhui yaliyowasilishwa katika riwaya, hasa ikizingatiwa kwamba baadhi ya riwaya zinatumiwa katika Mtaala wa Elimu nchini. Kwa hivyo, imebidi kufanya utafiti huu ili kurahisisha uratibu, uhakiki, upokeaji

na uelewekaji wa riwaya kwa walimu na wanafunzi. Katika kutimiza hili, utafiti umejikita katika kuchanganua maudhui, mtindo wa uandishi na wahusika katika riwaya.

Utafiti huu pia, umeonyesha namna riwaya inavyokua na kupata umbo jipya kimtindo.

Utafiti huu vilevile umefanywa kwa lengo la kuipa nguvu nadharia katika uchambuzi husika. Nadharia ya usemezo imedhihirisha kwamba kuna athari ya utenzi katika uandishi wa riwaya teule kimtindo.

1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Kuna vipengele vingi vya kimtindo katika kazi za kifasihi vinavyoweza kufanyiwa utafiti. Utafiti huu ulizingatia athari ya utenzi katika uandishi wa riwaya teule kama mbinu ya kimtindo katika fasihi. Hili lilifanywa ikizingatiwa kwamba kadri mtafiti anavyojua, hakuna utafiti ambao tayari umefanywa unaolingana moja kwa moja na utafiti huu.

Kuna riwaya nyingi ambazo zingeshughulikiwa katika utafiti huu. Hata hivyo, Utafiti umezingatia riwaya tatu; *Kasri Ya Mwinyi Fuadi*, *Walenisi* na *Msimu Wa Vipepeo*. Riwaya hizi zimeteuliwa kimaksudi kwa vile zina data toshelevu kwa utafiti huu. Aidha, utafiti umebainisha kwamba hizi riwaya ni vielelezo tu vya riwaya nyinginezo zenye sifa sawa. Kwa kila riwaya teule, vipengele vifuatavyo vya utenzi vimekuwa mwongozo katika kutathmini athari ya utenzi katika uandishi wa riwaya teule; maudhui, mtindo na wahusika.

Utafiti umejikita katika tenzi mbili; *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Utenzi wa Mwana Kupona*, Tenzi hizi zimeteuliwa kwa vile zina data toshelevu kwa utafiti huu, na tenzi hizi pia ni vielelezo tu.

1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Kuna maandishi mengi yaliyoandikwa kuhusu somo hili kwa upande wa nadharia, utenzi na riwaya. Mapitiyo ya kazi hizi yamesaidia kujenga mawazo ya utafiti kinadharia na kidata.

Utafiti mwingi uliofanywa kuhusu riwaya umejikita katika kuangazia vipengele mahsusi kama vile historia yake, maudhui, mtindo na wahusika. Hamna aliyechunguza athari ya utenzi katika uandishi wa riwaya kama mtindo wa uandishi, ambao ndicho kitovu cha utafiti huu.

1.6.1 Kuhusu Maudhui

Swaleh (1992), alishughulikia maudhui katika utenzi wa *Mwana Kupona*. Anasema kuwa maudhui ya dini yamejikita katika mafundisho ya dini ya kiislamu yanayomtunukia mwanamke nafasi anayostahiki katika jamii yake. Anaongeza kusema kwamba majukumu anayopewa mwanamke kwa jamii ndiyo yanachangia kumdhulumu. Tofauti na utafiti huu, ulichunguza matumizi ya maudhui ya dini katika riwaya teule kama taathira ya maudhui dini katika utenzi. Utafiti wa Swaleh uliufaa utafiti huu katika kubainisha vipengele muhimu vya kidini katika riwaya teule.

Anaye (2004) alitafiti kuhusu namna hadithi zilivyotumiwa kama chombo cha maudhui katika riwaya za Mkangi. Utafiti huu ulifaa kazi hii iliyoshughulikia maudhui katika

riwaya ya *Walenisi* cha Mkangi. Hata hivyo, utafiti huu unatofautiana na huo wa Anaye kwa ambavyo, utafiti huu ulijikita kwenye maudhui yaliyoko kwenye riwaya ya *Walenisi* ambayo yametokana na utenzi na siyo maudhui yote kwa jumla. Utafiti wa Anaye ulifaa utafiti huu kwa jinsi ambapo baadhi ya maudhui yaliyo kwenye riwaya ya *Walenisi* yalitokana na kazi ya Anaye.

1.6.2 Kuhusu Mtindo

Momanyi (1991) alishughulikia maudhui ya taswira kama kielelezo cha uhalisi katika *utenzi wa Al-inkshafi*. Katika utafiti wake, Momanyi alichunguza ni kwa namna gani, utenzi huu umebainisha mambo kwa uyaakinifu. Alishughulikia swala la historia ya mji wa Pate na amelinganisha na utenzi huu kufuatana na mambo yaliyotokea hasa. Pia aliangalia namna mazingira ya Pate yalivyomwathiri mtunzi hadi akachora taswira kadhaa kutokana na mazingira yake. Kwake Momanyi, taswira ni mbinu muhimu aitumiayo mtunzi katika kujenga maudhui yake. Tofauti na utafiti wa Momanyi, utafiti huu umemechunguza matumizi ya taswira katika riwaya teule kama taathira ya utenzi. Hata hivyo, utafiti huu ulinufaika na kazi ya Momanyi kutokana na undani wake wa kuzichambua taswira zinazojitokeza katika *utenzi wa Al-inkshafi*. Taswira ni moja ya mbinu za uandishi wa utenzi ambayo imetumika katika uandishi wa riwaya teule.

Kamau (1992), alichunguza ufundi katika riwaya za Mohamed Said Abdalla, alichunguza mbinu za uandishi kwa ujumla na vile zimetumiwa kuwasilisha maudhui ya mtunzi. Utafiti wake ni tofauti na huu, kwa vile utafiti huu ulijikita kwenye mbinu za uandishi wa utenzi na vile mbinu hizo zilivyotumika katika uandishi wa riwaya teule. Utafiti wa Kamau ulitufaa kwa namna ambavyo utatuelekeza kujua mbinu za uandishi kwenye

riwaya. Baada ya kuzijua mbinu hizi, utafiti huu utajikita tu kwenye zile mbinu ambazo zimo kwenye riwaya teule na ambazo zimetokana na utenzi.

Wamitila (2003) anasema kwamba sifa muhimu za tanzu za fasihi ni kwamba hujumulisha vikundi au vitanzu kadhaa. Anataja vitanzu katika utanzu mkubwa. Anasema kwamba, wakati wa urasimi kulikuwa na matumizi mengi ya uimbaji na nyimbo. Nyimbo ni mtindo wa kishairi kwa hivyo ushairi umetumiwa katika riwaya tangu urasimi. Aidha anasema kwamba uzungumzi wa wahusika katika riwaya siyo tu msingi wa usawiri wao, bali pia kielekezi cha dhamira na maudhui pamoja na ujenzi wa msuko. Utafiti wa Wamitila ulitufaa kwa kutuonyesha jinsi wahusika nguli wa utenzi wanavyojitokeza kwenye riwaya, pamoja na maudhui kadhaa kama ya ndoa, uongozi na dini.

Dalbak (2003) katika tasnifu yake *From The Epic to The Novel* anafafanua kwamba utenzi unaweza kubadilishwa na kuwa riwaya. Alitumia nadharia ya kiutanzu ya Bakhtin. Dalbak alihakiki utenzi wa *Beowulf* na vile uliandikiwa riwaya ya *Grendel* chake Gardener. Kilichobainika katika utafiti wa Dalbak ni kwamba utenzi ni utanzu wa fasihi ulio na sifa za kimonolojia, ilihali riwaya ni utanzu wa kipekee ulio na sifa za kiusemezo. Utafiti wa Dalbak ulikuwa wa msaada kwa utafiti huu hasa kwa upande wa kubainisha sifa za utenzi ambazo zimeathiri uandishi wa riwaya teule.

Kahara (2011) alishughulikia Tamthilia kama Utendi kwenye tasnifu yake ya uzamili. Utafiti huo wa Kahara unakaribiana na huu kwa vile unaonyesha vile utendi ulivyoweza

kubadilika na kuwa utanzu mwingine. Utafiti wa Kahara ulifaa utafiti huu kwa kuuchangia maelezo kuhusu historia ya utenzi wa Kiswahili na nadharia ya utafiti wenyewe. Tofauti ya utafiti wa Kahara na wetu ni kuwa huo ulishughulikia utendi ulivyobadilika na kuwa tamthilia mbili ambazo ni *Kinjeketile* na *Mzalendo Kimathi*. Utafiti huu ulishughulikia sifa za utenzi zilivyojitokeza kwenye uandishi wa riwaya teule: *Msimu wa Vipepeo* (Kyallo Wamitila), *Kasri ya Mwinyi Fuadi* (Adam Shafi Adam), *Walenisi* (Katama Mkangi).

Omutimba (2015) alishughulikia usimulizi katika riwaya za *Adili na Nduguze*, *Walenisi* na *Babu Alipofufuka*. Kwa mujibu wa Omutimba, usimulizi ni kipengele cha fasihi simulizi ambacho kimetumiwa kwenye fasihi andishi. Kipengele hiki kiliufaa utafiti huu hasa kwa vile miongoni mwa riwaya zinazotafitiwa ni ile ya *Walenisi*. Usimulizi pia ni miongoni mwa mbinu ya uandishi wa riwaya ambayo imetokana na utenzi. Maelezo muhimu kuhusu usimulizi katika riwaya ya *walenisi* yaliyotolewa kwenye utafiti wa Omutimba yaliufaa utafiti huu katika kuelewa zaidi kuhusu usimulizi.

1.6.3 Kuhusu Wahusika

Mberia (1989), alihakiki utenzi wa Fumo Liyongo kwa kutathmini sifa za Fumo Liyongo kama shujaa wa masimulizi. Tofauti na utafiti huu ambao umechunguza athari ya utenzi katika uandishi wa riwaya teule. Hata hivyo kazi hii ilitupa mwelekeo sifa za masimulizi na mashujaa wa utenzi katika riwaya teule.

Vutagwa (2013) alitafiti sifa za kiuhalisiaajabu na umuhimu wake katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Alijikita kuonyesha mambo yasiyokuwa ya kawaida ambayo hujitokeza katika utenzi huo. Pia anaonyesha wahusika wasiokuwa wa kawaida na jinsi wanavyotenda matukio yasiyo ya kawaida. Utafiti huo una uhusiano na utafiti huu hivi kwamba utafiti wetu pia utaangazia maudhui na wahusika wa utenzi na vile walivyojitokeza kwenye riwaya teule. Tofauti ni kwamba utafiti huu utazingatia tenzi mbili za *Fumo Liyongo* na *Utenzi wa Mwanakupona*.

1.6.4 Kuhusu Nadharia

Njogu (1993) aliyarekebisha madai ya Bakhtin (1981) kwa kuonyesha kuwa usemezo unaweza kuwepo katika ushairi simulizi wa fasihi ya Kiswahili. Alionyesha kuwa ushairi simulizi ni wa kiuusemezo kwa kuwepo na kushirikisha hadhira. Alionyesha pia kuwa sifa za riwaya zipo katika ushairi wa kiafrika, asema kama riwaya, ushairi huwa na kongamano la semi, sajili na lugha. Ushahidi wake aliutoa katika ushairi wa Afrika Mashariki wa Gungu, Kimondo na Gicaandi. Alifafanua jinsi tungo hizi zinavyodhihirisha usemezo. Sifa zote zilizopewa riwaya zilipatikana kwenye ushairi. Utafiti huu ulitufaa kuelewa kuwa usemezo uko katika fasihi ya Kiswahili, na kwa hivyo kutufaidi kuchunguza sifa za utenzi katika uandishi wa riwaya teule.

Karama (1996), alitafiti usemezo katika ushairi wa Kiswahili. Aliteua utenzi wa *Al-inkishafi* katika muktadha wa historia ya Pate. Aliangalia jinsi usemezo unavyoathiriwa na matukio ya kihistoria na unavyotegemea muktadha katika uelewaji. Utafiti huo ulitunufaisha katika kuelewa jinsi ya kutumia nadharia ya usemezo kama kipimo katika

utafiti wa fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo, utafiti wa Karama tofauti na huu ambao umetafiti usemezo wa utenzi na riwaya teule ya Kiswahili.

Naye Muriithi (2002), alifanya utafiti ili kubainisha kuwa usemezo unapatikana katika tamthilia ya Kiswahili. Alitumia tamthilia tatu ambazo ni *Mashetani* (Hussein, 1971), *Kilio Cha Haki* (Mazrui, 1981) na *Amezidi* (Mohammed, 1995). Katika utafiti wake, alionyesha kuwa kuna usemezo kwenye tamthilia ya Kiswahili. Alilenga pia kutanua nadharia ya usemezo katika muktadha wa fasihi ya Kiswahili. Utafiti wa Muriithi ulifaa kazi hii vile ulifafanua mengi kuhusu nadharia ya usemezano na ambayo utafiti huu umefaidi.

Kea (2006), alishughulikia usemezo katika nyimbo za Taarab. Utafiti wa Kea ulifaa utafiti huu kwa vile, unarejelea nadharia ya usemezo ambayo pia ilitumika katika utafiti huu. Mengi kuihusu mihimili ya nadharia hii yaliazimwa kutoka kwa utafiti wa Kea. Utafiti huu ni tofauti na huo wa Kea, kwa vile huu unahusu usemezo kwenye utenzi na riwaya teule bali huo wa Kea ulihusu usemezo kwenye nyimbo za taarabu.

Mohammed (2008) alishughulikia usemezano kama mkakati wa kufahamu riwaya za *Babu Alipofufuka* (2001), *Bina-adamu* (2002) na mkusanyiko wa Hadithi Fupi wa *Sadiki Ukipenda* (2002). Utafiti huo unaelekea kuwa sawa na huu kwa ambavyo riwaya zote zinashughulikia usemezo. Tofauti ni kwamba, utafiti huu ulirejelea usemezo wa utenzi kwenye riwaya teule za: *Msimu wa Vipepeo* (Kyallo Wamitila), *Kasri la Mwinyi Fuadi*

(Adam Shafi Adam), *Walenisi* (Katama Mkangi). Utafiti wa Bakari uliufaa utafiti huu kwa upande wa kuirejelea nadharia ya usemezo hasa mihimili yake.

1.7 Msingi wa Nadharia

Nadharia iliyotumiwa katika utafiti huu ni ya usemezo. Nadharia hii ilifaa kwa kuwa utafiti huu ulilenga kuchunguza sifa za usemezo kati ya utenzi na riwaya teule ya Kiswahili. Nadharia hii imehusishwa na mhakiki Mikhail Mikhailovich Bakhtin wa Kirusi. Mhakiki huyo aliandika kazi zake katika miaka ya baada ya mapinduzi ya Urusi ya mwaka wa 1917.

Bakhtin aliamini kuwa, kazi ya fasihi ina sauti mbalimbali zinazolingiliana na kupiga mwangwi katika kazi zingine zilizotangulia, zilizopo, au zitakazokuja baadaye. Hii ina maana kuwa matini yoyote ya kifasihi inafaa kuangaliwa katika muktadha wa kiusemezo. Kila matini huathiriwa na matini iliyotangulia, ilyopo au itakayofuata kama jibu au kikitikio.

Kuhusu usemezo, Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa matini ni uwanja ambao ni mwingiliano wa kiusemezo baina ya sauti mbalimbali za usemi. Kila matini inarejelea matini nyinginezo zilizopo, za wakati uliopita, na za wakati ujao.

Bakhtin (1981) alichukua msimamo kwamba nadharia hii ya usemezo ni pana mno, Kutokana na upana huu, nadharia hii ina mikondo ifuatayo;

- I) Wengi lugha.
- II) Utohatima.

- III) Mwingiliano matini.
- IV) Kani-pewa na Kani-kitovu.
- V) Kronotopu.
- VI) Kanivali.

Mikondo hii yote imejadiliwa moja baada ya nyingine na ilikuwa mihimili muhimu ya kuchanganua data katika utafiti huu. Mkondo uliotiliwa maanani sana katika utafiti huu ni ule wa kani pewa na kani kitovu ambao tumeujadili kwa mapana na marefu.

Kwa mujibu wa Bakhtin, mkondo wa kwanza ambao ni kani kitovu unashikilia kuwa, maneno yanayopatikana katika matini zozote za kifashi huwa ni kama elementi za kiutendaji zilizopo katika uhusiano wa kiusemezo. Elementi hizi hufanya kazi yake katika viwango mbalimbali. Kuna kiwango cha upinzani kati ya 'kani pewa` ambazo hujaribu kuvitenganisha vitu na 'kani kitovu' ambazo hujaribu kuvioanisha. Utenzi ni utanzu unaopatikana katika kiwango cha kani kitovu, hii ni kwa sababu una umbo maalum linalotambulika. Umbo hili ni kama vile; mishororo mifupi, mistari minne katika kila ubeti, na baadhi ya tenzi zina `bahari`.

Tenzi nyingi zina maudhui maalum na mtindo ulio sawa wa uandishi. Tenzi ni chache sana ambazo zimechapishwa kwa miaka ya hivi karibuni, kwa vile kulingana na utafiti wetu baadhi ya watunzi wa tenzi hizo, sasa wamejikita katika uandishi wa riwaya. Mfano ni waandishi Adam Shafi na Said Ahmed Mohamed ambao badala ya kutunga utenzi ambao ni asili ya kwao, hivi sasa wamebobeza katika uandishi wa riwaya. Riwaya ambazo wameandika kwa kutumia sifa za utenzi, ni kama; *Kasri ya Mwinyi Fuad* (Shafi Adam)

na *Utengano* (Said Ahmed Mohamed). Utenzi ni utanzu wa fasihi uliofungika kimtindo hivyo kuunga mkondo wa utendaji wa kani kitovu.

Riwaya ni utanzu ambao umejikita kwenye kiwango cha kani pewa. Hii inatokana na sababu kwamba, riwaya za Kiswahili zimejitokeza katika maumbo tofauti tofauti, ama riwaya hizi hazifanani. Kuna riwaya ambazo ni za kipelelezi, kuna zile za kijazanda, kuna zile zinazorejelea dini na ndoa miongoni mwa nyingine. Utanzu wa riwaya umebadilika hata kwenye mbinu za uandishi. Waandishi kama Ken Walibora wametumia misimbo ya kiwakati katika uandishi wao. Ken Walibora ametunga riwaya kwa kutumia lugha ya Sheng. Katika riwaya ya *Kidagaa Kimemuozea*, Walibora anamchora mhusika Bob Dj akizungumza lugha ya Sheng na akina Amani na Imani.

Bakhtin anashikilia kwamba, riwaya haina pingamizi nyingi ulizonazo ushairi. Hii ni kwa sababu riwaya hutumia lugha ya kawaida katika kuyawasilisha maudhui ya mtunzi. Ni kweli kwamba kila tamko liko pekee yake, lakini kila lugha huzoeleka kutumiwa katika mawanda fulani hadi matamshi haya yakajimakinisha katika mawanda mahususi. Kulingana na Bakhtin lugha hizi huweza kuitwa sajili.

Suala la sajili ladhihirisha kwamba matamshi yana mfumo, lakini Bakhtin hatoi mfumo huu kutokana na nadharia yake. Kwake, maana imefungika katika muktadha na muktadha haukufungika. Huku kutofungika kwa matamshi ndiko akuitako 'ndimi za usemi'. Huku kutofungika kwa matamshi kunatokana na makisio ya usemezo kwamba kila neno huathirika kiwakati, mahali na pia huwa na nguvu fulani zinazodhibiti neno hilo. Bakhtin

(1981), anapendekeza. kwamba riwaya pekee ndiyo sajili mwafaka kwa sababu lugha yake nzima imo katika usemezo. Anasema kwamba lugha ya ushairi kuanzia mwanzo hadi mwisho ni kama mtu mmoja azungumzaye wala hakuna ushirika wowote. Katika ushairi mshairi tu ndiye asemaye wala hamna anayemjibu mshairi kwa sababu lugha ya ushairi haikubali mwingiliano wowote wa wasemezwa.

Kwa upande wa lugha ya riwaya, Bakhtin anasema kwamba ndiyo pekee yenye kuchanganya sajili zote kwa pamoja, ndiyo pekee yenye kukubali maingiliano na hadhira yake. Pia lugha ya riwaya ndiyo pekee yenye kujuza kwamba kuna wahusika wawili wanaoshirikiana katika kusemezana na ndipo riwaya inaendelea kusemezana na utenzi kimaudhui, kimtindo na kiwahasika.

Michael Holquist (1990), akijadili maoni ya Bakhtin kuhusu usemi, anasema kwamba semi zote za kimaumbile ni za kusemezano. Hii ina maana kuwa, kila semi ni jibu la kitu kingine na hutarajiwa kujibiwa. Anasisitiza kuwa usemezano una sifa za kutokamilika. Hii ni kwa sababu hakuna kauli ya mwisho, kwani semi zote za kusemezo huwa na uwili wa mwelekeo na mkabala. Utafiti huu umedhihirisha kuwa semi ambazo zinapatikana kwenye riwaya teule za *Kasri ya Mwinyi Fuad, Walenisi na Msimu wa vipepeo* zimesemezana na semi nyingine katika utenzi. Holquist anakubali kwamba, matini zote lazima ziwe zahusiana lakini anasisitiza kwamba riwaya pekee ndiyo yenye kutumainia kuathiriana. Kwa muhtasari pia Holquist aligusia swala la historia katika usemezo na kuonyesha umuhimu wa historia katika kufahamu maana na kufaidika na kazi za kifasihi. Kwa hivyo historia inatiliwa mkazo katika usemezo.

Dhana nyingine muhimu katika nadharia hii ya usemezo ni ‘kanivali’. Bakhtin analitumia neno ‘kanivali’ kurejelea sherehe za kitamaduni ulaya ambapo watu hujivisha maguo na mafigu yanayozisitiri sura zao. Katika hali hii, watu hao hufanya sarakasi na matendo ambayo huenda kinyume na matendo ya kawaida au yanayokubalika. Mhakiki huyu alisema kuwa matendo ya kanivali ni ya kiucheshi na yalikusudiwa kuwa kijalizo cha utamaduni wa kimwinyi. Licha ya tofauti zinazoonekana, matendo hayo yote huwa sehemu ya utamaduni mmoja wa ucheshi wa kanivali.

Mwanda wakati au ‘Kronotopu’ ni kipengele muhimu katika nadharia ya usemezo. Bakhtin alitumia dhana hii kuzieleza sifa muhimu au bainifu za wakati wa mwanda au mahali katika tanzu mbalimbali. Katika kiwango cha usemi, neno huwa na maana fulani kutegemea historia ya lugha na hali tofauti za wakati huo huo wa kihistoria. Mwanda-wakati hii inaakisi wakati wa kinadharia usioelekea kuwa na athari za kisaikolojia au kibayolojia kwa wahusika.

Mukarovsky (1977) alitoa tofauti iliyopo baina ya usemezo na uzungumzi wa mtu mmoja. Kwa upande wa uzungumzi wa mtu mmoja, anasema kwamba kiisimu humanisha yale maneno ya mtu mmoja tu bila kutilia maanani kuweco au kutokuweco kwa washiriki wengine katika mazungumzo hayo. Mukarovsky anatoa sifa tatu za usemezo. Sifa hizi zatokana na mahusiano yaliyopo baina ya washiriki wawili. Washiriki hawa hutambuana kama ‘mimi’ na ‘wewe’ na wakati wa mazungumzo yao majukumu ya msemaji na msikilizaji hubadilishana mara kwa mara. Aidha kuna mahusiano ya washiriki wa mazungumzo na mazingira waliomo. Mazingira haya huathiri moja kwa moja mwelekeo wa mazungumzo. Uhusiano wa tatu ni ule wa muktadha wa usemezo.

Muktadha hufafanua taratibu na maana ambazo hubainishwa kwa urejelezi tofauti katika mazungumzo. Kwa hivyo riwaya zilizoteuliwa katika utafiti huu zimedaiwa kuathiriwa na utenzi kwa kurejelea baadhi ya mbinu za uandishi hususan matumizi ya uzungumzi nafsia. Kuna matumizi mengi ya uzungumzi nafsi katika riwaya hizi ambayo ni athari iliyotokana na utenzi.

Wingi sauti ni kazi za fasihi zinazoonyesha sauti tofauti zilizo huru. Wahusika hasa wale wakuu huwa na sauti ambazo zina mamlaka sawa na sauti ya msimulizi ambayo inahusika kwa kiasi kikubwa katika usemezano na sauti za wahusika hawa. Sauti hairejelei msemaji tu bali pia yale mahusiano ya nguvu ambayo humwathiri na kumweka msomaji katika hali fulani.

Mwingilianomatini ni kimelea cha nadharia ya usemezo. Nadharia hii iliasisiwa na Julia Kristeva (1980). Kristeva aliamini kuwa, mwingilianomatini ni uzalishaji wa maana ndani ya matini na wala siyo ndani ya mahusiano kati ya matini mbalimbali. Matini huzaliwa kutokana na unukuzi unaotokana na matini tangulizi, mahusiano ndani ya matini husika na matini nyingine. Kila matini au usemi hudokeza mahusiano ya matini tangulizi, kupitia kwa unukuzi wa matini iliyopitwa na wakati. Kwa hivyo, tanzu zinaingiliana kimatini katika kukamilishana na ni vigumu kuziwekea mipaka bayana. Katika utafiti huu, neno ‘mwingilianomatini’ limetumiwa kwa maana ya njia mojawapo inayotumiwa kujenga masemezano baina ya utenzi na riwaya teule. Hapa tanzu za utenzi na riwaya zinachanganyikana hivi kwamba zile za awali (utenzi) kuathiri zile za baadaye (riwaya) kimaudhui, kimtindo na kiwahasika.

Utafiti ulitumia mihimili ifuatayo;

- i) Kani-pewa na kani-kitovu ambao ni upinzani baina ya kauli hizi. Kani –pewa hutenganisha maandishi ama masimulizi na kani-kitovu ambayo huleta mshikamano katika maandishi au masimulizi. Muhimili huu ulitumika kuonyesha kuwa ni riwaya teule ndiyo ilipata athari ya sifa za utenzi.
- ii) Katika kiwango cha usemi, neno huwa na maana fulani kutegemea historia ya lugha na hali tofauti za wakati huo kihistoria. Muhimili huu ulitumika kuonyesha kuwa ingawa maudhui ya dini, malezi na ndoa yalisawiriwa katika utenzi, usawiri wake katika riwaya teule ni tofauti kutokana na mabadiliko ya jamii.
- iii) Kila matini ina maana ambayo inaifungamanisha na matini zingine. Mhimili huu ulitusaidia kutumia mtazamo linganishi kusawiri ujumbe.
- iv) Athari zinazopatikana kutokana na matamshi ya msembeza (utenzi) na msembezewa (riwaya) hurejelea matini iliyotumika. Mhimili huu ulisaidia kubainisha kuwa riwaya teule ni taathira ya utenzi kwa sababu matini husemezana.

1.8MBINU ZA UTAFITI

1.8.0 Muundo wa Utafiti

Muundo wa utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo. Huu ni mtazamo ambao huchunguza sifa zinazobainika katika jambo linalochunguzwa. Dhima yake ni kuchunguza hali ya mambo na jinsi mambo hayo yalivyo katika mazingira fulani. Lengo kuu katika muundo huu huwa ni kukusanya data na kubainisha uhusiano baina ya vigezo husika. Kupitia kwa muundo huu maelezo muhimu kuhusu utenzi yamejadiliwa na kisha kueleza jinsi umeathiri uandishi wa riwaya teule.

1.8.1 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa maktabani ambapo usomaji wa kina wa vitabu, tasnifu, majarida na marejeleo mengine kuhusu mada yalifanywa. Usomaji huu wa maktabani ndio ulitufaa ili kupata yaliyoandikwa kuhusu mada, na ulituwezesha kupata pengo la utafiti ambalo ni mtindo wa uandishi wa riwaya ambao umetokana na utenzi. Vile vile ni kutokana na usomaji wa maktabani ambapo data muhimu kuhusu mada, ambazo ni maudhui, mtindo na wahusika waliotokana na utenzi na jinsi wameathiri uandishi wa riwaya, ilipatikana pamoja na kuboresha misingi ya nadharia iliyotuongoza katika utafiti. Ni maktabani pia ndipo tulipata kuteua mbinu za utafiti wetu huu.

1.8.2 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli iliteuliwa kimaksudi. Usampulishaji wa kimaksudi ni mbinu ambapo, sampuli huteuliwa kwa misingi ya malengo ya mtafiti. Mtafiti analazimika kuteua sampuli kimaksudi kwa vile, akitumia njia nyingine atapata sampuli isiyofaa utafiti wake. Mtafiti kwa hivyo, hulazimika kuteua kimaksudi sampuli ambapo kwa maoni yake anafikiri itamfaa. Katika utafiti huu, sampuli lengwa ilikuwa riwaya tatu teule: *Kasri ya Mwinnyi Fuadi, Msimu Wa Vipepeo na Walenisi*, na tenzi mbili; *Utenzi wa Fumo Liyongo na Utenzi wa Mwana Kupona*. Mtafiti alitaka kutumia sampuli hizi kuangazia athari za utenzi katika uandishi wa riwaya teule kama mbinu ya kimtindo katika uandishi wa kinathari.

1.8.3 Njia ya Ukusanyaji Data

Data ilikusanywa kwa kusoma wa kina wa riwaya teule tatu: *Kasri Ya Mwinyi Fuadi, Msimu Wa Vipepeo na Walenisi*. Kwa kutumia kalamu na karatasi mtafiti alinukuu mambo muhimu kuhusu mada ya utafiti. Uhakiki wa kina ulifanywa. Usomaji wa riwaya hizo ulifanywa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya usemezo. Data pia ilipatikana kwa kusoma majarida na vitabu vingine vya ziada. Njia hii ya usomaji ilitumiwa ili kupata vipengele na sifa bainifu katika riwaya hizo teule za Kiswahili, na kuonyesha utaratibu unaohusika katika uandishi wa riwaya kwa kutumia sifa za utenzi kwa kunukuu sehemu katika riwaya teule zenye sifa za utenzi.

1.8.4 Uchanganuzi wa Data

Data ilipangwa kwa kuzingatia maudhui, mtindo na wahusika. Kisha, data hii ilichanganuliwa kwa kuzingatia, maudhui ya riwaya teule yanavyowiana na utenzi, kuonyesha mtindo wa utenzi unavyowiana na mtindo wa uandishi wa riwaya, kubainisha wahusika wa riwaya teule walivyowiana na wale wa utenzi. Haya yote ni kwa sababu ya kutaka kuliziba pengo la utafiti ambalo ni kuonyesha athari za utenzi katika uandishi wa riwaya teule ya Kiswahili. Uchanganuzi pia ulilenga kujibu maswali yaliyohusiana na utafiti huu kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya usemezo.

1.8.5 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo na utoaji mifano mwafaka. Maelezo yalitolewa katika sura tano zifuatazo; Pendekezo, Maudhui, Mtindo, Wahusika, na Hitimisho.

1.9 Kiishilio

Sura hii imeshughulikia utangulizi wa utafiti huu kwa jumla kama mwongozo wa mchakato wa utafiti huu. Mtafiti alijadili mada ya utafiti ambayo ni mchango wa utenzi katika uandishi wa riwaya ya Kiswahili. Aidha, alionyesha maswali na malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada na upeo na mipaka ya utafiti. Misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada, mbinu za utafiti na pia ukusanyaji na uchanganuzi wa data ni mambo yaliyofafanuliwa katika sura hii. Sura inayofuata inashughulikia athari ya maudhui ya utenzi katika uandishi wa riwaya teule ya Kiswahili.

SURA YA PILI

2.0 Athari Ya Maudhui Ya Utenzi Katika Riwaya Teule

2.1 Utanguliizi

Sura hii imechunguza athari ya maudhui ya utenzi katika riwaya teule. Katika hali hii, historia na maendeleo ya utenzi na riwaya imejadiliwa. Historia ni kiungo muhimu cha jana leo na kesho (Bakthin 1990). Ufafanuzi wa kihistoria katika sura hii ni muhimu kwa kuwa umeonyesha uwiano na mwingiliano wa maudhui katika utenzi na riwaya teule. Hali hii inawiana na kipengele cha nadharia iliyouongoza utafiti huu kinachoeleza ya kuwa matini huzaliwa kutokana na unukuzi unaotokakana na matini tangulizi, mahusiano ndani ya matini husika na matini nyingine.

2.2. Historia na Maendeleo ya Utenzi na Riwaya

Historia ina umuhimu mkubwa (Hiloquist 1990). Fasihi ya Kiswahili ina umbo lake maalum ambalo ni lazima lieleweke katika muktadha maalum wa kihistoria ya jamii (Mulokozi 1999). Kwa hivyo, kuchunguza historia ya utenzi na riwaya ni muhimu kwa sababu kumewezesha utafiti kuonyesha kati ya utenzi na riwaya ni kipera kipi kilitangulia. Hivyo, ilisaidia kubainisha athari ya kimaudhui baina ya utenzi na riwaya.

Utenzi ni utanzu mmojawapo wenye historia ndefu katika ushairi wa fasihi ya Kiswahili (Wamitila 2002); Foibe (2013) wanabainisha kwamba upana huu wa kihistoria wa utenzi ndio umesababisha ugumu wa watafiti mbalimbali kuuzungumzia.

Kulingana na Finnegan (1970), tenzi nyingi zilizotungwa kabla ya majilio ya wageni katika bara la afrika zilikuwa zikikaririwa kwa vinywa tu kabla ya majilio ya maandishi.

Mulokozi (1999) anaeleza kuwa ingawa utenzi wa Fumo Liyongo ulitungwa mwaka wa 1813 na Mohamed Kijumwa kuna idhibati ya kuonyesha kuwa kisa cha Liyongo kilikuwa kikisimuliwa kabla ya kuandikwa katika bahari ya utenzi.

Wanyela (2007) anaeleza kuwa utenzi kama ushairi wa Kiswahili unahusishwa na kipindi cha urasimi. Anaendeleza kusema kuwa utenzi ulikuwepo katika masimulizi kabla ya maandishi. Baadhi ya tenzi zilizoandikwa katika kipindi cha urasimi ni: *Utenzi wa Tambuka* (Chuo cha Herekali 1728), *Utenzi wa Hamziya*, *Utenzi wa Fumo Liyongo* (1813). Awamu hii ya utenzi ndiyo iliyowekea msingi wa ushairi andishi. Ni baada ya kuchipuka kwa maandishi ndipo riwaya iliibuka. Kwa hivyo utenzi una historia kongwe kuliko riwaya ya Kiswahili.

Madumulla (2009) anaeleza kwamba riwaya ilitokana na nathari bunifu simulizi kama vile utenzi, hekaya na hadithi iliyosimuliwa kwa mdomo. Katika hali hii, imebainika kwamba riwaya ilitokana na maandiko ya fani ya ushairi hasa utenzi wa Kiswahili.

Utafiti ulibainisha kuwa riwaya ikiwa kani pewa kulingana na nadharia iliyoongoza utafiti huu, chimbuko lake lipo katika mambo makuu mawili ambayo ni fani za kijadi za fasihi kama vile utenzi ambao ni kani kitovu pamoja na mazingira ya kijamii. Kwa mujibu wa Mulokozi, fani hizi za kijadi ni masimulizi na ndipo zikapata kuigwa na watunzi wa riwaya.

Maelezo ya kihistoria yalikuwa ya muhimu kwani yamesisitiza ufafanunzi wa Holiquist (1990) ambaye ni mmoja wa waitifaki wa nadharia ya usemezo, kuwa historia ni muhimu

katika usemezi kwa sababu husaidia kufahamu maana na kufaidika na kazi za kifasihi. Kwa hivyo historia inatiliwa mkazo sana katika usemezo.

2.3 Maudhui ya Utenzi Katika Riwaya Teule

Tenzi nyingi za Kiswahili zinafanana kidhamira na kifani (Wamitila 2002). Asilimia kubwa ya tenzi za Kiwahili zimeshamiri maudhui ya dini, ndoa na malezi. Maudhui ni jumla ya maswala yote muhimu ambayo hujidhihirisha katika kazi yoyote ya kifasihi na ambayo hufafanuliwa na mtunzi akitumia uwezo wake wote kuyaendeleza. Maswala haya muhimu ni yale yanayotokana na jinsi mtunzi anavyokuza mada ambayo ni msingi wa utunzi wa kazi yake. Kwa mujibu wa nadharia ya usemezo, matini zote lazima ziwe zahusiana lakini riwaya pekee ndiyo yenye kutumainia kuathiriana ili ipate kubakia jinsi ilivyo. Hata hivyo, utafiti ulibainisha kwamba si riwaya tu ndiyo hutegemea sana uathiriano wa matini, bali lugha nzima yategemea uathiriano. Hivyo basi, lugha nzima imo katika uathiriano riwaya ikiwemo kama aina moja ya matumizi ya lugha.

Mtunzi yeyote wa fasihi ana uhuru wa kuchunguza na kuzungumzia jambo lolote bora lichukuane na matarajio yake pamoja na uzoefu wa jamii husika (Masinde 2003). Akifanya hivyo, mtunzi atakuwa amechota malighafi yake kutoka mandhari ya jamii husika. Utenzi na riwaya kama tanzu za fasihi zimekuwa na uwezo mkubwa kumulika maswala anuai yamhusuyo binadamu na Mungu wake na mtagusano wake na mazingira anamoishi. Hivyo, maudhui ya dini, ndoa na malezi ambayo yalishamiri katika tenzi nyingi za Kiswahili ndiyo yanaangaziwa katika riwaya za Kiswahili. Maudhui haya yamejidhihirisha wazi katika riwaya teule za *Kasri ya Mwinyi Fuad, Walenisi na Msimu wa Vipepeo*.

2.3.1 Dini Katika Riwaya Teule

Utafiti ulibainisha kuwa tenzi nyingi za awali ziliegemea dini ya Kiislamu. Watunzi walibainisha Mungu kama chanzo cha utunzi wao. Aidha tungo zao zilishamiri maudhui na masuala yanayohusu dini ya Kiislamu. Hali hii inauweka utenzi kuwa kani kitovu kwa sababu inazingatia dini moja kuu. Kwa upande mwingine, watunzi wa riwaya katika riwaya teule wamezingatia dini. Hata hivyo, wameegemea dini ya Kiislamu, Kikristo na dini za asili. Hali hii ya riwaya kuzingatia dini tatu tofauti inatilia nguvu mhimili wa ‘kani pewa’ katika nadharia uliyouongoza utafiti huu kwani hamna njia moja ambayo waandishi wa riwaya hutumia katika utunzi.

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, maudhui ya dini yanajidhihirisha wazi pale tunapomuona Julia ambaye ni mkewe waziri Mkurutu akikimbilia waganga ili wamsaidie kuirekebisha ndoa yake ambayo ilikuwa inayumbayumba. Katika ukurasa wa 104, Julia anasema kuwa alitaka kwenda njia ya kuelekea kwa mganga ambaye angemsaidia na mbinu za kujinasua kutokana na mabawa ya shida na mateso. Anasema. “...waganga wa kuweza kuwasaidia waliolemewa na matatizo ya ndoa na kuuhui moto wa mapenzi ambao ulikuwa unafifia.”

Aidha, katika hali ya mawazo, tunaona Julia akikumbuka kwamba akiwa mtoto, alifunzwa kwenye madarasa ya Biblia kwamba ni bora kuwa na imani kubwa ili uweze kukabiliana na matatizo duniani. Kutokana na hali hii, anajisuta kutokwenda kwa waganga na badala yake aweke imani yake kwa mwenyezi Mungu. Pia katika riwaya, tunabaini kupitia kwa mwandishi kuwa Julia alikuwa mshiriki wa kwaya kanisani.

Katika ukurasa wa 113, Melissa anakumbuka kuwa nyanyake alikuwa mshirikina. Anasema kuwa nyanyake alikuwa na mazoea ya kutia maji kwenye mkebe na kuwapa

wajukuu wake wote wanywe kwa imani kuwa wakinywa maji hayo yatawalinda dhidi ya ya wachawi na itawawezesha kusoma hadi ulaya.

Usawiri wa maudhui ya dini katika riwaya hii ya *Msimu wa Vipepeo* umechukua mkondo wa utenzi. Katika *Utenzi wa Mwana Kupona*, Mwana Kupona anaweka imani yake yote ya uponyaji kwa mwenyezi Mungu. Mwana Kupona anamuomba Mungu amuondolee ndwele mbovu. Kwa mujibu wa Ndung'o (1985) Mwana Kupona aliugua ugonjwa wa tumbo kutoa damu. Huu huwa ni ugonjwa wa kivimbe katika sehemu ya uzazi. Dua lake kwa mwenyezi Mungu katika ubeti wa 78 anaposema: "...Nondolea ndwee mbovu..." ubeti wa 79: "...nepulia uvukuto..." ubeti 80 "...Unondolee makhafu..." ubeti (85) "...nyingi takalufu..." linaonyesha mawazo ya mashaka, masumbuko na wasiwasi yaliyotokana na ukosefu wa dawa za kuuwa viini vya ndwele kama hiyo iliyokuwa ikitunga ndani na kusababisha kushikwa na homa. Kwa mujibu wa El- Maawy (2011) huu ndio "uvukuto" ambao Mwana Kupona aliomba uondoke.

Hali sawa na hii inajitokeza katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* ambapo tunaona Julia akiamini kuwa mganga (dini asili) ndiye angeweza kurutubisha ndoa yake na waziri Mkurutu.

Kazi ya Julia kushiriki katika uimbaji wa kwaya kanisani na kuhudhuria madarasa ya Biblia ni hali ya kujitolea kumtumikia mwenyezi Mungu. Kwa hivyo suala hili la utumishi kwa mwenyezi Mungu lilikuwepo katika utenzi na hivyo likaathiri utenzi wa riwaya ikiwemo ya *Msimu wa Vipepeo*.

Vile vile, katika riwaya ya *Walenisi* tunaona kuwa Dzombo alipoingia anga za juu alikuwa na hisi kuwa ameiwacha nyuma Jehanamu na kuingia mbinguni. Katika hali hii,

Dzombo anawaza kuhusu mwenyezi Mungu na atakavyomwambia afikapo mbele yake. Anajawa na maswali mengi kuhusu Mungu.

Uoga wa Dzombo kumkabili Mungu unatokana na siku ya kيامa ambapo katika dini inaaminika kwamba mtu anapofika huenda kwa mwenyezi Mungu ili ahukumiwe. Masuala haya ya kيامa na hukumu pia yanajitokeza katika tenzi za awali. Katika *Utenzi wa Mwana Kupona* tunaona Mwana Kupona ubeti wa 24 mtunzi anasema “...Naawe radhi mumeo, Siku zote mukao...” ubeti wa 25: “...Na ufapo... wenda uitukuzie, ndipo upatapo ndia...” ubeti wa 26: “...Siku ufufuliwao, nadhari nda mumeo...” na ubeti wa 27: Kipenda wende peponi... kinena wende motoni, huna budi utatiwa...”

Suala la majilio ya mwenyezi Mungu pia linajitokeza. Tunaeleza kuwa kijana Mtu-Tabia alimuuliza Dzombo kuhusu kuwasili kwa mwenyezi Mungu kwa sababu majilio yake yalitabiriwa. Hata hivyo Dzombo anamsisitizia Mama-Mtu kwamba kwa maanani yeye si Mungu wala hakuna Mungu duniani kinyume na imani ya wenyeji. Baada ya muda ilibainika kuwa Dzombo alitoka Jehanamu kutokana na usemi wake kuwa lugha ya atokako ni “English” nao (Waliokuwa sayarini) wakatafsiri “ilblish” wakasema hiyo lugha ya Dzombo ni ya ibilisi shetani. Suala hili linaoana na utenzi wa Fumo Liyongo ambapo baada ya mwanaye Liyongo kushawishiwa na mfalme na kisha kumuua babake, mfalme anafananisha kitendo hicho cha kumuua babake na ibilisi. Ubeti wa 214 unasema:

... Usiketi mui wangu
wewe adui ya Mungu...

Kutokana na hali kuwa riwaya ni “kani pewa” kulingana na usemezo, dini katika riwaya ya *Walenisi* imetumiwa vibaya na wadhalimu. Walioko duniani kama chombo cha

kuwanyanyasa wanyonge. Wanyonge wanaelezwa kuwa wavulimilie shida za sasa lakini watakata raha kule mbinguni baada ya kufa. Wachuna wanafahamisha watawaliwa kwamba kuzaliwa maskini ni majaliwa ya Mungu na hivyo faraja yao waingoje baada ya kifo.

Mawazo haya ya kutumia dini kama chombo cha kudhulumu wengine hayamo katika tenzi. Hata hivyo yanaendelezwa katika riwaya kwa kufuata mkondo wa utenzi. Mabadiliko haya yanatokana na mabadiliko ya kijamii, kihistoria na kiuchumi katika jamii ya sasa. Mabadiliko haya yanatokana na ukweli kuwa msanii hutunga kazi kulingana na mazingira na masuala yanayoathiri jamii yake.

Hata hivyo, Mkangi kupitia *Walenisi* anaendelea kushughulikia kipengele cha dini jinsi utenzi kama vile wa Mwana Kupona na Fumo Liyongo umeshughulikia. Tenzi hizi zilichukulia kuwa kila binadamu yuko sawa mbele ya mwenyezi Mungu.

Walenisi kwa upande wao walionelea kuwa Mungu anapenda watoto wote. Hivyo hawezi kamwe kumfanya mmoja tajiri na mwingine masikini. Mungu hana ubaguzi hata kidogo. Kwa hivyo, Wawalenisi wanaamini Mungu ni mapenzi, na mapenzi yake lazima yatimizwe hapa duniani kama ilivyo kule mbinguni. Mwono huu ni sawa na ule wa utenzi wa Mwanakupona katika ubeti wa 61 ambapo Mwana Kupona anamuusia Binti Hashima awapende na awaheshimu watu wote. Mishororo ya kwanza miwili ya ubeti huu inasema:

...Watu wote waumini,
kwako na wawe wendani...

Kusali au dua ni muhimu katika dini ya Kiislamu (Swaleh 1992). Utunzi wa riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* sawa na utenzi wa Fumo Liyongo na Mwana Kupona umeshamiri masuala ya dini ya Kiislamu. Tunaelezwa katika uk 14 kuwa “...ilipofika magharibi, baada ya kwisha kusali Fuad aliteremka...” pia katika ukurasa wa 15 tunaona mzee Shurwani akimuaga Fuad ili aende kusali. Hii inaonyesha jinsi jamii ya Adam Shafi ilivyotilia maanani dini hasa kipengele cha maombi kwa mwenyezi Mungu. Sifa hii ya umuhimu wa kusali au maombi inajitokeza wazi katika utenzi. Kwa kawaida tenzi nyingi zilianza kwa maombi na kufunga kwa maombi. Kwa mfano katika utenzi wa Fumo Liyongo mtunzi anaanza katika ubeti wa kwanza kwa kusema:

Bismilahi nabutadi
kwa ina la Muhammadi
nandikie auladi
nyuma watakaokuya ...

Hapa mtunzi anaomba dua mwenyezi Mungu amwezeshe kutunga utenzi huu ili vijana watakaokuja baadaye pia waweze kuusoma. Pia utenzi wa Mwana Kupona sawa na riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* unasisitiza mafunzo ya dini ya Kiislamu, kumtii Mungu na mtume wake, kupenda na kutenda haki. Katika ubeti wa 12 mshororo wa kwanza, Mwana Kupona anasema, “... la kwanda kamata dini...”

Utafiti ulibainisha kwamba, utunzi kuhusu maombi katika dini ya Kiislamu ulikuwepo katika tenzi kabla ya kuingizwa katika riwaya za Kiswahili. Kwa hivyo, Adama Shafi aliathirika pakubwa na kazi za utenzi katika utunzi wa riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* kuhusu dini ya kiislamu hasa kipengele cha maombi. Hali hii ya riwaya kuathirika na maudhui ya dini yanakubaliana na mhimili wa nadharia ya usemezo kuwa, tanzu huingiliana kimatini katika kukamilishana na ni vigumu kuziwekea mipaka bayana.

2.3.2 Malezi Katika Riwaya Teule

Malezi ni kumkuza mtu au mtoto kwa kuzingatia taratibu zilizokubalika kupitia makuzi, lishe, ulezi na uangalizi (Mdee 2012). Aghalabu malezi ni njia ya ukuzaji wa mtoto kwa kutarajia afuate tabia na mwenendo unaostahiki. Kwa ufafanuzi huu, yeyote asiyefuata mienendo inayokubalika na jamii hajapata malezi mazuri na hivyo kuchukuliwa kama aliyekiuka maadili katika jamii.

Uzazi na malezi ni masuala yanayokaribiana sana. Tenzi nyingi za kale zilitungwa kwa kuzingatia suala la malezi. Katika tenzi kama vile *Utenzi wa Mwana Kupona* na *Fumo Liyongo*, imebainika kwamba malezi ya watoto aghalabu ni jukumu la wazazi hasa mwanamke au mama. Kwa mujibu wa Hoogvelt (1976) hali ya kumchukua mwanamke kama mlezi ni jukumu la mwanamke kulingana na itikadi na utamaduni wa jamii za Kiafrika.

Suala la malezi sawa na lilivyoendelezwa kati katika tenzi, limeshughulikiwa katika riwaya. Hali hii inakubaliana na nadharia ya usemezo kuwa matini huzaliwa kutokana na unukuzi unaotokana na matini tangulizi.

Watunzi wa riwaya sawa na utenzi wameshughulikia maudhui ya malezi kwa kusawiri malezi bora na malezi duni miongoni mwa jamii. Katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, Shafi anasawiri malezi duni kwa watoto. Shafi anaanza riwaya hii kwa kutupa taswira ya Bw. Malik and mkewe Bi. Maimuna ambao walikuwa wamejaliwa na mtoto wa kiume aitwaye Fuad. Fuad alilelewa kwa kudekezwa na wazazi wake. Tunaona Maimuna akifurahia anapomuona Fuad akimuamrisha Kijakazi. Katika uk 2, mtunzi anasema,

“... Fuad alikuwa mtoto mkubwa mwenye umri wa miaka mitano na mtundu wa kutosha. Kutwa alikuwa anavunja vitu ndani ya nyumba na alipenda kusema chochote mbele ya mtu yeyote, na katika yote haya hakuna aliyeweza kumkanya kuchelea kutukanwa na Bw. Malik au na Bi. Maimuna. Alidekezwa kupita kiasi na kila alilofanya lilikuwa sawa mbele ya wazee wake...”

Malezi haya duni kwa Fuad yaliendelea hadi wazazi wake walipoaga dunia na kumwacha yatima. Shafi anaonyesha kuwa malezi haya mabaya yalimfanya Fuad kutumia mali aliyoridhi kutoka kwa babake vibaya. Kwa kutumia kisengere nyuma tunaarifiwa jinsi Bw. Malik alihifadhi mali na pesa zake tofauti na Fuad ambaye amezitumia kununua gari la kifahari ili awe maarufu mjini. Aidha tunaona kuwa Fuad anaendeleza ujeuri huu wa utotoni hadi utu uzima na kushindwa kumpata mke. Malezi katika riwaya ya Kasri ya Mwinyi Fuad ni kinyume cha malezi katika *Utenzi wa Mwanakupona* na *Fumo Liyongo*. Hali hii ya utofauti inatokana na kipengele cha nadharia ya usemezo kuwa matini za kifasihi huwa katika elementi za kiutendaji zilizopo katika uhusiano a kiusemezo ambazo hufanya kazi katika viwango mbalimbali ambavyo ni kani pewa na kani kitovu, kanipewa hujaribu kuvitenganisha vitu na kani kitovu hujaribu kuvionanisha. Kwa hivyo uhusiano wa malezi katika utenzi na riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* ni wa kani kitovu na kani pewa ambapo utenzi ni kani kitovu nayo riwaya ni kani pewa.

Tunapata kuwa *Utenzi wa Mwana Kupona* tofauti na riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* unamuonya Binti Hashima ambaye ni mtoto wake Mwana Kupona umuhimu wa kuwa na mahusiano mema na watu katika jamii. Mwana Kupona ambaye anatoka katika tabaka la juu kama vile la Fuad na jamii yake anamfahamisha bintiye umuhimu wa utangamano na wanajamii wengine.

Kwa upande mwingine, Bw. Malik na Bi. Maimuna katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* hawataki kamwe Fuad atangamane na watu wengine akiwemo mlezi wake Kijakazi. Tunaona kuwa hata baada ya Fuad kuwa anampenda Kijakazi, Bi. Maimuna anamwonya dhidi ya kutangamana naye.

Aidha, suala la malezi limejitokeza katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* kupitia mhusika Ndumi. Tunapata kuwa Julia ambaye ni mamaye Ndumi anatalikiana na mumewe Bw. Kanda kutokana na umasikini. Baadaye Julia anaolewa kwa Bw. Mkurutu ambaye alikuwa mwanasiasa. Katika hali hii, Ndumi anapata malezi ya baba wa kambo. Ndumi hakuyafurahia malezi ya aina hii na kupelekea hata kumuulizia mamake kuhusu babake. Hali hii inaendelea hivyo hadi pale Ndumi hatimaye anakutana na babake Bw. Kanda baada ya muda mrefu. Aidha tabia ya Ndumi ilivyoanza kubadilika na akaanza kutofanya vizuri shuleni, tunaona Julia anafuatilia kwa walimu ili afahamu jinsi mtoto wake anaendelea. Julia anamwonya Ndumi dhidi ya marafiki wabaya.

Malezi ya aina hii yanawiana na yaliyomo katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* ambapo baada ya mtoto wa Liyongo kuja na kumuuliza liyongo namna anaweza kuuwawa. Liyongo anamuonya mtoto wake kuwa huenda anatumiwa na mahasimu wake na watamtumia na kisha kumuacha akiumia. Pia, katika ubeti wa 47, tunaarifiwa kuwa Liyongo alimlea vizuri na kumpenda mtoto wake.

Vile vile suala la malezi limejadiliwa katika riwaya ya *Walenisi*. Katika riwaya hii, tunaona Dzombo anapofika nchi ya Walenisi anakutana na familia ya mzee Mtu Mwenzio na mkewe Mama Mtu Maanani. Kutokana na tabia za watoto wao mtu binti Fikirini, Hekima na wavulana wawili Mtu Wazo na Mtu Tabia, tunaona kuwa hii ni

familia ambayo ina mfano wa malezi ya kupigiwa mfano katika jamii. Kila mtoto alipewa malezi bora na aliwajibika kwa kile alichokifanya katika jamii. Kwa mfano, Mtu Binti Fikirini akiwa mkurugenzi wa kiwanda cha kutengeneza Trimi, anaifanya kazi hiyo kwa bidii. Hali hii inatokana na malezi mazuri yenye uwajibikaji katika jamii.

Kwa hivyo, ni wazi kuwa utenzi ukiwa kani kitovu umeathiri pakubwa riwaya ambayo ni kani pewa kupitia maudhui ya malezi ambayo yalijitokeza hapo awali katika utenzi na kuendelezwa katika riwaya jinsi yalivyo katika riwaya teule.

2.3.3 Ndoa Katika Riwaya Teule

Asasi ya ndoa ndiyo huendeleza ukuaji wa jamii (Masinde 2003). Hii ina maana kuwa ndoa ndiyo msingi wa familia na jamii. Katika dini ya Kiislamu na Kikristo, ndoa ni asasi ambayo mwasisi wake ni Mungu.

Tenzi nyingi za Kiswahili ukiwemo *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Utenzi wa Mwana Kupona* zimeshughulikia suala la ndoa. Watunzi wa riwaya wamefuata mkondo uo huo wa utenzi ambapo wanaongelea masuala tofauti katika ndoa katika jamii ya sasa. Masulala haya yamechotwa katika utenzi na kuendelezwa katika riwaya.

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* kunatokea ndoa baina ya Kanda na Julia. Ndoa hii inadumu kwa miaka kumi na mitano na kisha kuvunjika. Jambo linalosababisha kuvunjika kwa ndoa hii ni umasikini katika familia ya Julia na Kanda.

Julia anaamua kumtaliki Kanda kwa ajili ya umaskini unaowakumba na kurudi kwa wazazi wake hata baada ya kuzaa naye mtoto aitwaye Ndumi. Hatua hii ya Julia inakinzana na *Utenzi wa Mwana Kupona* ambao ni kani kitovu kwani Mwana Kupona

alimuusia bintiye kuwa aheshimu kile kidogo alichu nacho mumewe. Aliarifiwa azingatie uwezo wa mumewe bila kutaka mambo au vitu ambavyo mumewe hangeweza kuvimudu.

Wosia huu unakinzana na ndoa ya Julia ambaye baada ya kumtaliki Kanda anapata mchumba mwingine aitwaye Bw. Mkurutu ambaye wanafunga naye ndoa. Bw. Mkurutu alikuwa mwanasiasa ambaye alikuwa na mali. Hata hivyo, ingawa Julia aliolewa kwa waziri Mkurutu anapitia changamoto nyingi katika ndoa hii. Tunaona (uk.19) Julia akilalamika kuwa ingawa mwaka umepita tangu ndoa yake na Mkurutu, bado hajamjua na kumuelewa mumewe. Anajiuliza iwapo wanawake na wanaume wote walioolewa hupitia mtihani huu. Ndoa hii ilikuwa na machungu mengi kwani hata baada ya upasuaji Julia hakufaulu kumpata mtoto. Ilijidhihirisha wazi katika riwaya hii kuwa utajiri sio chanzo cha maisha mazuri katika ndoa. Kwa upande mwingine, ndoa kati ya mzee Kitali na Nzasika ni ya maelewano. Wazee hawa wanaishi maisha ya kimaskini lakini kuna mapenzi ya dhati baina yao. Hali hii inajidhihirika tunapomuona mzee Kitali akimshughulikia mkewe alipokuwa mgonjwa kwa kumtafutia dawa za kienyeji na kumtibu nazo.

Aidha katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* kuna ndoa baina Bi. Maimuna na bwana Malik. Wawili hawa wanaishi kwa kupendana. Tunaelezwa kuwa wawili hawa walipenda kustarehe kwenye bustani pamoja. Vile vile katika riwaya ya *Walenisi* kuna ndoa kati ya Dzombo na Binti Fikirini ambao wanaoana baada ya ziara ya Dzombo kule kwenye nchi ya Walenisi. Mwandishi anatarifu kuwa hata Dzombo alipowaza kurudi katika nchi yake, mkewe alikuwa mjamzito. Utafiti ulibainisha kwamba suala la ndoa katika riwaya ni jambo ambalo watunzi wamelichukua kutoka utenzi. Kwa mfano utenzi mzima wa *Mwana Kupona* unaongelea suala la ndoa ambapo Mwana Kupona anamshauri bintiye

Hashima namna anaweza kuishi na mumewe na wanajamii akiwa katika ndoa. Aidha katika utenzi wa Fumo Liyongo tunaona Liyongo akifunga ndoa na mkewe aliyozwa na Wagalla ambaye walizaa naye mtoto wa kiume. Kwa hivyo, maudhui ya ndoa katika riwaya ni kani pewa nao utenzi ni kani kitovu. Uhusiano huu unatokana na watunzi wa riwaya kuendeleza maudhui ya ndoa ambayo ndiyo pia yalishughulikia katika utenzi. Kwa hivyo, maudhui ya ndoa katika riwaya yanatokana na athari ya utenzi ambao ulishughulikia suala hili la ndoa hapo awali kabla ya riwaya.

2.4 Kiishilio

Sura hii imetalii athari ya maudhui ya utenzi katika riwaya teule. Tulichunguza na kudhihirisha jinsi maudhui ambayo yalitumika katika utenzi yana taathira katika riwaya teule. Utafiti umeonyesha jinsi maudhui ya dini, malezi na ndoa ambayo yalishamiri tenzi mbalimbali ukiwemo utenzi wa *Mwana Kupona* na wa *Fumo Liyongo* yameathiri utenzi wa riwaya teule. Utafiti ulibainisha kwamba maudhui ya dini, ndoa na malezi katika riwaya teule ni taathira ya utenzi. Aidha utafiti umebainisha umuhimu wa historia katika usemezo. Kwa hivyo, historia katika usemezo husaidia kuelewa maana na kufaidika na kazi za kifasihi. Sura inayofuata inashughulikia athari ya mtindo wa utenzi katika riwaya teule.

SURA YA TATU

3.0 Athari ya Mtindo wa Utenzi Katika Riwaya Teule

3.1 Utangulizi

Sura hii imeangazia athari ya mtindo wa utenzi katika riwaya teule. Imechunguza athari ya vipengele vya mtindo wa utenzi kama vile usimulizi, uunganifu na matumizi ya taswira. Kuchunguza athari ya mtindo wa utenzi katika riwaya ni muhimu kwa sababu mtindo ndio huonyesha kufaulu au kutofaulu kwa mtunzi (Senkoro 1982). Mtindo humbainisha mtunzi na kazi yake katika kuchora dhamira na maudhui yake (Momanyi 1991). Maelezo haya yanashahibia na nadharia inayouongoza utafiti huu kwamba katika usemezo, mtindo huathiriana kutoka tanzu hadi tanzu bila kubadilika tanzu hiyo. Kwa hivyo, matumizi ya mtindo wa utenzi katika riwaya hayabadilishi utanzu wa riwaya.

Senkoro (2011) akielezea kuhusu mtindo anasema mtindo katika kazi ya fasihi ni ile namna ambayo mtunzi hutunga kazi husika na kuipa sura ambayo kifani na kimaudhui huainisha kanuni zilizofuatwa kama ni za kimapokeo au za kipekee. Kwa hivyo, kupitia mtindo wa utenzi tunaweza kubainisha sifa za kimapokeo za utenzi katika riwaya. Kwa mtazamo wa nadharia ya usemezo, mtindo wa utanzu mmoja unaweza kutumiwa katika kuwasilisha utanzu mwingine. Kauli hii inaoana na ufafanuzi wa Wamitila (2006), kuwa utanzu wa riwaya unaweza kuingiza vipengele vya tanzu nyingine lakini ukabaki na sifa zake kama riwaya.

Fasihi ni sanaa ambayo hutumia lugha kiubunifu (Wellek na Warren, 1949). Ubunifu wa mtunzi hubainika kupitia uchunguzi wa mtindo ambao umetumiwa na mtunzi katika kazi yake.

Mtunzi hutumia mtindo fulani kwa madhumuni ya kupitisha ujumbe wake kwa njia inayoeleweka. Kwa hivyo matumizi ya mtindo wa utenzi katika riwaya ambayo ndiyo kani pewa katika utafiti huu hutegemea falsafa ya mtunzi mwenyewe, nyakati, mazingira na aina ya ujumbe anaotaka kuwasilisha.

Kwa mujibu wa (Mulokozi 1996), mtindo wa riwaya haukuzuka hivi hivi tu bali ulitokana na fani za kijadi za masimulizi kama vile utenzi. Kwa hivyo, kutokana na maelezo ya Mulokozi mtindo wa riwaya ya Kiswahili unaiga mtindo wa fani za utenzi. Utafiti huu umechunguza matumizi ya mtindo wa usimulizi, uunganifu na taswira katika riwaya teule.

3.2 Usimulizi Katika Riwaya Teule

Usimulizi ni kipengele muhimu katika utenzi (Mulokozi 1996). Riwaya za Kiswahili zilizoteuliwa kwa utafiti huu pia zimetumia mtindo wa kimasimulizi. Baadhi ya riwaya zimetumia masimulizi ya kihistoria. Kwa mujibu wa (Wamitila 2003) masimulizi ya kihistoria ni masimulizi ya mwanadamu katika muktadha wa wakati, na ni fani muhimu katika jamii. Masimulizi ya kihistoria yanaweza kuwa ya mdomo au maandishi na huwa chemichemi nzuri ya riwaya.

Riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* ni mfano wa riwaya ya masimulizi ya kihistoria. Shafi anatomia mbinu ya masimulizi kwa kutusimulia jinsi Waafrika katika kisiwa cha Zanzibar walipigana dhidi ya ukoloni wa wamwinyi na mabwana. Anasimulia jinsi Waafrika waliungana ili kupigana na umwinyi na baadaye kushinda na kuanzisha ujamaa.

Ndung'o (1985) akimukuu Mulokozi (1982) anafafanua kuwa maingiliano kati ya wageni kutoka Bara Hindi na Waafrika ndiyo yalianzisha umwinyi Uswahilini. Tabaka la

matajiri lilijitokeza kutokana na maingiliano ya wenyeji wa Afrika hususan kisiwa cha Zanzibar na wageni kutoka Bara Hindi. Maisha ya wageni hawa yaliimarika kutokana na hali yao ya uchumi. Hali hii ilipelekea wageni hawa kuishi maisha bora kuliko wenzao walioishi kando ya miji. Ni harakati hizi ndizo, chanzo cha jamii zenye umwinyi katika upwa wa Afrika mashariki.

Kutokana na uwezo wao wa kiuchumi, wageni hawa matajiri walinunua ardhi kubwa ambapo walihitaji waafrika wawafanyie kazi katika hayo mashamba. Hali hii ndiyo ilisababisha mgawanyiko wa kitabaka ambapo wafanyikazi katika mashamba wakawa kwenye tabaka la chini na wageni matajiri wakawa katika tabaka la juu.

Tabaka tawala lilikuwa lile lenye ardhi nao wafanyikazi wakawa tabaka la watwana ambao walifanya kazi katika mashamba ya matajiri ili kupata riziki. Tabaka hili la wafanyikazi lilionewa, kugandamizwa na kunyanyaswa kule kazini.

Kupitia kwa masimulizi katika *Kasri ya Mwinyi Fuad*, Shafi anatusimulia kuwa hadhi ambayo familia ya bwana Malik na Bi. Maimuna inawakilisha wamwinyi matajiri waliowanyasya wafanyikazi. Kwa upande mwingine Kijakazi, Vuai, Mkongwe, Mariam na wafanyikazi wengine wanawakilisha tabaka la chini.

Shafi anatumia mtindo huu wa masimulizi kwa kuonyesha historia ya kuundwa kwa Ujamaa na harakati ambazo Waafrika walitumia ili kujinasua kutoka katika unyanyasaji wa wamwinyi.

Mtindo wa masimulizi ya sira pia umetumika. Sira ni masimulizi ambayo ni ya kweli kuhusu habari za maisha ya mtu zikisimuliwa na mtu mwingine au ziwe tawasifu ya habari ambayo mtu mwenyewe binafsi anasimulia kuhusu maisha yake. Kulingana na

ugunduzi wa utafiti huu, sira ambayo ilitumika katika utenzi simulizi iliathiri kuchipuka kwa riwaya hasa inapoonyesha masimulizi ya maisha ya mtu toka utotoni hadi uzeeni.

Katika riwaya ya teule ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, usimulizi kuhusu maisha ya Fuad ni mfano wa masimulizi ya sira. Katika riwaya hii, Shafi anatusimulia maisha ya Fuad kuanzia azaliwe, kulelewa akiwa na Kijakazi kama mlezi hadi anaporithi mali ya wazazi wake Bw. Malik na Bi. Maimuna. Shafi anataeleza jinsi Fuad alidekezwa na wazazi wake akiwa mtoto. Malezi haya yanamfanya hata anashindwa kupata mke na badala yake anaanza kuwanyemelea wafanyikazi wake wa kike kama vile Mariam na Mkongwe. Mtunzi anatumia jinsi Fuad alivyotumia vibaya mali na kuwatesa wafanyikazi. Anakamilisha kazi yake kwa kutuonyesha hatima ya Fuad ambapo wafanyikazi wanatekeleza mapinduzi na kuanzisha ujamaa ambapo ardhi na mali yote ya Fuad inachukuliwa na kugawanywa wafanyikazi. Tunaona namna Fuad anasononeka kutokana na hali hii. Hadithi hii kumhusu Fuad inaelezwa kupitia mtindo wa masimulizi.

Aidha, riwaya ya *Walenisi* inaakisi masimulizi ya wasafiri. Masimulizi ya wasafiri hueleza habari zinazosimulia masaibu ya wasafiri katika nchi mbalimbali. Katika riwaya teule ya *Walenisi*, tunaona kuanzia sura ya kwanza Dzombo akipewa sayari kama chombo cha kuenda kumwangamiza. Tofauti na vile ilitarajiwa, Dzombo anakitumia kifaa hiki vizuri na kukiendesha hadi kinapompeleka katika ulimwengu mwingine. Mkangi anatusimulia safari ya Dzombo katika huu ulimwengu mpya wa Walenisi. Tunasimulia jinsi alisafiri kwa trimi sehemu mbalimbali. Pia tunasimuliwa safari yake ya kurudi kwao duniani alikokuita Jehanamu.

Masimulizi katika riwaya hizi teule sawa na masimulizi katika riwaya *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Mwana Kupona*, unaakisi masimulizi ya kihistoria, sira na safari. Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* tunasimuliwa kisa cha Liyongo tangu utotoni wake hadi kifo chake. Kijumwa anatusimulia historia ya uongozi wa jamii ya Liyongo. Kupitia utenzi huu, anatumia kwamba, kwa kuwa babake Fumo Liyongo alikuwa ameaga dunia, uongozi ulipaswa kupokezwa hadi kwa watoto wake.

Vile vile *Utenzi wa Mwana Kupona* umetungwa kupitia mtindo wa masimulizi. Mwana Kupona kupitia utenzi huu kwa bintiye anasimulia jinsi bintiye Hashima anastahili kuishi katika ndoa. Pia anasimulia aina ya maradhi ambayo yanamkumba. Kutokana na maelezo haya hapo juu kuhusu masimulizi, ni wazi kwamba mtindo wa riwaya ya Kiswahili ni taathira ya utenzi. Riwaya ndiyo kani pewa kwani imetumia aina mbalimbali ya masimulizi ambayo yanatokana na masimulizi ya utenzi ambao ni kani kitovu katika muktadha huu.

3.3. Uunganifu Katika Riwaya Teule

Utenzi lazima uwe na msuko na mfuatano wa kimantiki wa visa (Ndumbaro 2013). Ndumbaro anauita mtindo huu kuwa ni wa uunganifu. Riwaya za Kiswahili zimeakisi mtindo huu. Utafiti ulibaini kwamba riwaya ya *Walenisi*, *Kasri ya Mwinyi Fuad* na *Msimu wa Vipepeo* zina uunganifu na mtiririko wa visa vyenye mantiki.

Uunganifu katika riwaya teule ya *Walenisi* unatokea pale mwanzo mwa riwaya ambapo tunakutana na Dzombo akiwa ameletwa mahakamani kwa tuhuma za uchochezi na utovu

wa nidhamu kwa utawala. Hakimu anatoa hukumu ya kifo kwa Dzombo ambacho kingetekelezwa kwa sayari.

Katika hatua ya pili, Dzombo anaingia kwenye sayari kungoja kifo chake. Tunaona safari yake ya muda mrefu iliyokuwa na changamoto tele. Dzombo anafaulu kukwepa kifo kilichokuwa kimemkodolea macho kutokana na ujuzi aliokuwa nao. Dzombo anasafiri na kufika nchi ya Walenisi ambapo alilakiwa vyema na wenyeji na kuona maendeleo nchi yao.

Dzombo alifanya utafiti wake na kugundua kuwa katika nchi hii, kulikuwa na Wachuna ambao hapo awali walimiliki mali yote ya jamii na kuwatesa wanajamii kwa muda. Hata hivyo, baadaye jamii ilizinduka na kuwang'oa mamlakani wachuna wote na kuleta ujamaa na maendeleo ambapo mali yote ilitaifishwa. Dzombo alipogundua siri hii, anaamua kurudi duniani ili kubadilisha jamii na kuleta maendeleo.

Utafiti ulibainisha kuwa sawa na utenzi, riwaya ya *Walenisi* imeunganika kimatukio kutoka mwanzo hadi mwisho. Ilibainika kuwa ingawa kuna urejeshi nyuma na mbele, suala na uunganifu limetiliwa maanani.

Aidha katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, uunganifu unajitokeza kwa kuwepo mtiririko wa matukio ambayo yamepangwa katika sura tatu ndefu. Riwaya hii imejengwa kwa familia ya Bw. Malik ambaye alikuwa tajiri wa kutajika. Riwaya inaanza kutuonyenya Malik na Maimuna wakiwa wanabarizi katika bustani. Wazazi hawa walibarikiwa na mtoto mmoja aitwaye Fuad.

Katika maendelezo, riwaya inatuonyesha maisha ya wazazi wake Fuad na jinsi alivyodekezwa. Tunafahamishwa kuhusu kifo cha wazazi wa Fuad ambaye alichukuliwa

na kulelewa na rafiki wa babake hadi alipofika umri wa mtu mzima aliporithishwa mali ya babake. Shafi anatuonyesha jinsi Fuad aliwanyanyasa wafanyikazi na hata yeye mwenyewe kushindwa kuoa.

Katika maendeleo haya, wafanyikazi walishindwa kuvumilia dhuluma za mabwana shamba na kuamua kuleta mapinduzi katika utawala wa Kisultan. Wafanyikazi hawa walipigana vita vikali na baada ya kupata ushindi walijenga jamii mpya yenye kudhamini ujamaa. Walitaifisha mashamba yote na yakawa mali ya umma. Fuad alikuwa mmoja wa wale walioadhirika na hivyo shamba na mali yake ikachukuliwa na kutaifishwa.

Vile vile riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* inaakisi uunganifu. Riwaya nzima inafafanua maisha ya Julia katika ndoa. Riwaya inianza kwa kutuonyesha ndoa ya kwanza ya Julia na Kanda ambayo imevunjika. Tunafahamishwa sababu ya kuvunjika kwa ndoa ya kwanza kuwa ni umaskini. Katika hali hii, mtunzi anaturejesha katika ndoa ya pili ya Julia kwa waziri Mkurutu. Kwa kutumia mbinu ya kisengere nyuma, Wamitila anajaribu kulinganisha maisha ya Julia katika ndoa hizi mbili.

Suala la Ndumi ambayo ni mtoto wa Julia na Kanda linajitokeza. Tunaona changamoto katika ndoa ya pili ya Julia zinasababisha Ndumi kutamani babake Bw. Kanda. Tunaona kuwa baada ya Julia kufurahia ndoa yake ya pili kwa muda mfupi, waziri Mkurutu alianza kuwa na jicho la nje. Hali hii ilipelekea Julia kuwa na upweke kiasi kwamba Ndumi, bintiye anagundua kuwa mamake ana huzuni mwingi. Tunaona Julia akijuta kutokana na kuondoka kwake katika ndoa yake na Kanda.

Kufikia mwisho wa riwaya, tunamuona Ndumi akiwa ametafuta babake na kumfahamisha kuhusu maisha ambayo mamake alikuwa anayapitia kule kwa Mkurutu.

Katika hali hii, Ndumi anampa mamake nambari ya simu ya babake ili waanze kuwasiliana tena.

Uunganifu ulikuwepo katika utenzi kabla ya riwaya. *Utenzi wa Mwana Kupona na Fumo Liyongo* ni kielelezo kizuri cha uunganifu katika utenzi. Maelezo katika tenzi hizi yamepangwa kimantiki. Katika *Utenzi wa Mwana Kupona* tunaona mtiririko wa matukio kuanzia mwanzo hadi mwisho. Katika utenzi huu, Mwana Kupona anaanza kwa kumuita bintiye ana jambo la kumwambia.

Katika kuendeleza kwake, mtunzi anaeleza nia yake. Mwana Kupona anaanza kumfahamisha bintiye kuhusu maisha ya ndoa jinsi ya kuishi na mume na jamii. Akielekea kumaliza, mtunzi anafahamisha bintiye azingatie yote aliyomwambia. Hatimaye anakamilisha kwa dua. *Utenzi wa Fumo Liyongo* umefuata mtindo uo huo ambapo mtunzi anaanza kwa kuomba mwenyezi mungu amsaidie katika utenzi na kuendeleza masimulizi hadi mwisho ambapo pia anashukuru mwenyezi Mungu.

Utafiti ulibainisha kuwa mtindo wa uunganifu katika riwaya ya Kiswahili ni taathira ya utenzi. Hivyo mtindo huu umezimwa kutoka utenzi na kuendelezwa na watunzi wa riwaya za Kiswahili. Chambilecho nadharia ya usemezo, mwingilianomatini ni uzalishaji wa maana ndani ya matini bali siyo ndani ya mahusiano kati ya matini mbalimbali. Kauli hii inaoana na maelezo ya Kristeva (1980) kuwa matini huzaliwa kutokanana na matini tangulizi, mahusiano ndani ya matini husika na matini nyingine.

3.4 Matumizi ya Lugha

Lugha ina mchango mkubwa katika kazi ya fasihi. Lugha ndiyo huleta utofauti baina ya fasihi na sanaa nyingine kama vile, uchongaji, ufinyanzi na uchoraji. Kwa mujibu wa Senkoro (1982) lugha katika fasihi ndiyo malighafi inayotumiwa kuundia sanaa hiyo.

Lugha ina mchango mkubwa katika fasihi kwa kuwa fasihi ni lugha. Lugha huweza kubainika aidha moja kwa moja au kwa nia ambayo sio ya moja kwa moja (Wamitila 2003). Kwa hivyo, uwasilishaji wa maudhui na dhamira katika utenzi na riwaya kama tanzu za fasihi hutegemea pakubwa jinsi lugha ilivyotumika. Katika utafiti huu, matumizi ya taswira katika riwaya teule yamejadiliwa.

3.4.1 Taswira

Taswira ni yale maelezo yanayojenga picha, jambo au hali akilini mwa msikilizaji au msomaji (Wamitila (2003). Mbinu za sitiari na tashbihi husaidia pakubwa katika kujenga taswira. Taswira katika utenzi sawa na riwaya humsaidia pakubwa msomaji katika kuelewa mazingira au mandhari na vitu vinavyoonekana. Katika hali hii msanii hutilia msisitizo na mkazo kauli ambazo tayari zimeshatolewa. Kwa mujibu wa nadharia iliyouongoza utafiti huu, hakuna usemi ambao mtu anaweza kumtoa na aseme yeye ni wa kwanza. Kwa hivyo, matumizi ya lugha katika riwaya jinsi ilivyoendelezwa katika utenzi ni suala ambalo linaeleweka. Kulingana na Bakhtin (1986) matamshi yote ni majibu. Utafiti ulibainisha kwamba kila anayesema jambo huwa anatarajia jibu. Vivyo hivyo, mtunzi huichora taswira fulani ili watu wapate funzo na wajiepushe na lile lenye kuleta hasara.

Katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, mtunzi anaanza kwa kutuchorea taswira ya jumba la Bw. Malik na kutupa picha ya utajiri wake. Mtunzi katika (uk. 1) anasema "... Jumba la Bw. Malik lilikuwa... kubwa na la fahari, halina mfano wake jirani. Vyumba vyake vingi, waliojua ni watumishi wa ndani..."

Aidha, Shafi anatupa picha jinsi Bw. Fuad alitaka kumnyemelea Mkongwe katika chumba chake akiwa amelewa chakari. Katika riwaya hii, matumizi ya taswira yameshamiri sana. Katika kurasa za 12 na 17, mtunzi anatupa picha kamili ya urembo wa Mariam na Mkongwe ambao walikuwa wafanyikazi katika shamba la Fuad (uk 17), Mtunzi anasema "... Mkongwe alikuwa mzuri wa maumbile. Mashavu yake yalikuwa ya duara, nywele zake nyeusi... zependaza sana. Na nguo alizokuwa amevalia, huonyesha vizuri vifua vyao vilivyo jaa kwa maziwa ya ujana wao..." katika nukuu hili, msomaji anapata picha ya msichana mrembo licha ya kuwa mfanyikazi wa kufanya kazi za sulubu katika shamba la Fuad.

Katika riwaya ya *Walenisi Katama Mkangi* anatupa taswira kamili ya duniani ambayo anafananisha na Jehanamu. Hali hii inatokana na mateso yanayopatikana duniani. Anatupa picha ya mahakamani ambako Dzombo anahukumiwa kifo bila kosa linaloakisi hukumu hiyo. Pia kupitia mhusika Dzombo mtunzi anatupa taswira ya Walenisi. Tunaona Dzombo anapofika huko anakaribishwa vyema. Katika hali hii, nchi ya Walenisi inatupa taswira ya ulimwengu huru. Aidha, mtunzi anarejelea viongozi kuwa kama popo. Katika hali hii anatupa picha ya ndege ambaye ana sifa za kuwa mnyama na ndege. Kupitia kwa neno hili, mkangi anatupa taswira ya viongozi wabaya wasiosimamia upande wowote.

Vile vile riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* imetumia mbinu hii ya taswira. Wamitila anaanza katika (uk. 1.) Kwa kutupa mazingira alimokuwa Julia na hali yake Julia wakati huo. Mtunzi anaanza kwa kusema:

“... Harufu ya chavu ya maua, sauti za ndege na mkorongo... ulipenya dirishani hadi chumbani alimokuwa. Matawi yalicheza na kupigana pambaja na upepo... Julia, uso wenye mashavu yaliyojaa vidu umechanuka, macho yameng’aa na tabasamu kuvaa uso mzima...”

Kupitia maelezo haya msomaji anapata picha ya mazingira aliyomo Julia. Matumizi ya taswira yametumika na mtunzi wa riwaya hii hapa na pale na hivyo kuchukuliwa kama mbinu muhimu ya usanii wake.

Momanyi (1991) anabainisha kuwa utenzi hujengwa kutokana na mbinu ya taswira. Anabainisha *Utenzi wa Fumo Linyongo* kama utenzi ambao umesheheni matumizi ya taswira, kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kwa mfano mtunzi anatufahamisha kuhusu sifa za Linyongo kwa kutupa picha ya sifa za ajabu. Kwa mfano, katika ubeti wa 37, 38 na 39 kupitia kwa maelezo ya mtunzi tunapata picha ya Linyongo kama mtu wa ajabu, mwenye nguvu na mwenye kustaajibisha kutokana na jinsi aliwasili pate na vitu alivyobeba. Ubeti wa 37 unasema:

Mkobani akatowa
zitu alizotukuwa
nyumba ndima nisikiya

Kupitia ubeti huu, msomaji anapata ya picha Fumo Linyongo alivyokuwa na nguvu zisizo za kuwaida. Taswira hii inajitokeza kutokana na vitu vingi alivyokuwa amevibeba ambavyo tunafahamishwa vingejaa nyumba nzima.

Utafiti ulibainisha kuwa taswira ilikuwa kipengele muhimu katika utunzi wa dhamira na maudhui katika utenzi. Matumizi ya taswira yaliendeleza na kupanuliwa na watunzi katika riwaya teule. Hii inatokana na ukweli kuwa matini husemezana.

3.5 Kiishilio

Uchunguzi kuhusu mtindo wa utunzi ni muhimu (Msokile 1993). Sura hii imedhihirisha kwamba matumizi ya mtindo wa usimulizi, uunganifu na taswira katika riwaya teule ni taathira ya utenzi. Utafiti ulibainisha kuwa mtindo katika fasihi huathiriana kutoka tanzu moja hadi nyingine. Hata hivyo, athari hii haisababishi tanzu moja kubadilika, hadi nyingine. Kwa hivyo athari ya mtindo wa utenzi katika riwaya teule haubadilishi riwaya kuwa utenzi. Hii ina maana kuwa mtindo wa utanzu mmoja unaweza kutumiwa kuwasilisha utanzu mwingine.

Sura inayofuata imeshughulikia athari ya wahusika wa utenzi katika riwaya teule.

SURA YA NNE

4.0 Athari ya Wahusika Majagina wa Utenzi Katika Riwaya Teule

4.1 Utangulizi

Sura hii imechunguza athari ya wahusika hususan majagina wa utenzi katika riwaya teule. Aidha wahusika majagina ambao ni wahusika nguli katika riwaya teule na ni taathira ya wahusika wa utenzi walibainishwa na kufafanuliwa. Utafiti katika sura hii pia umebainisha changamoto ambazo wahusika majagina katika riwaya hupitia katika safari zao. Changamoto hizi na mitego zimeangaliwa katika riwaya teule kwa kuonyesha kuwa ni taathira ya utenzi. Athari ya wahusika majagina wa utenzi katika riwaya inaakisi ukweli wa nadharia ya usemezo kuwa tanzu moja huchota malighafi kutoka nyingine ili kudhihirisha dhamira na maudhui ya mtunzi (Bakhtin 1990).

4.2 Taathira ya Wahusika Majagina wa Utenzi Katika Riwaya Teule

Wahusika ni watu au mtu, wanyama, mimea, vitu na wadudu anaotumia mtunzi katika uwasilishaji wa kazi kwa hadhira. Kulingana na Msokile (1993), utenzi wa Kiswahili una sifa ya kuchanganya wahusika binadamu na wale wasio binadamu. Utafiti ulibainisha kwamba sifa hii ya kuchanganya wahusika pia imetumika katika riwaya teule.

King'ei na Kemoli (2001) wamefafanua wahusika kama viumbe, vitu au watendi wanaotumiwa na mshairi katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake. Katika maelezo yao, wanasema kwamba mshairi huwatumia wahusika kwa nadra sana, isipokuwa katika tenzi na mashairi ya masimulizi. Uchunguzi huu ulitambua umuhimu wa wahusika katika kusawiri matukio ya utenzi na riwaya teule.

Uteuzi wa wahusika katika kazi za fasihi huchangiwa na mambo tofauti. Utafiti ulibainisha kuwa watunzi wengi wa utenzi wa Kiswahili hutunga kwa kuzingatia ufunuo na matatizo yanayowakumba wakati huo au kulingana na mkondo wa mabadiliko na wakati wake. Hivi ni kumaanisha kwamba, tenzi zilitungwa kwa kuongozwa na matukio katika jamii anamoishi mtunzi. Changamoto ambazo zinawakumba wanajamii wa mtunzi kutokana na mabadiliko haya hudhihirishwa kupitia wahusika waliomo katika tenzi za wakati huo. Aidha anaweza kutabiri mambo yatakayokuja badaye na hivyo kuyaakisi kupitia wahusika wake.

Wamitila (2003) anafafanua kuwa wahusika wakuu wa utenzi huwa ni majagina. Anafafanua utenzi kama shairi refu la kisimulizi linalozungumzia kwa mapana na kwa mtindo ambao ni wa hali ya juu. Aidha Mulokozi (1996) anafafanua utenzi kama utungo mrefu ambao husimulia matukio ya kishujaa yenye uzito wa kijamii au kitaifa. Kwa hivyo, wahusika ambao hutegemewa na mtunzi wa utenzi ni wahusika majagina.

Kwa mujibu wa Gichamba (2005), jagina ni mtu ambaye humiliki uwezo zaidi kuliko uwezo wa watu wa kawaida na hutumia uwezo huu kiujasiri na huwa na uwezo wa kuyahafanisha maisha yake kwa manufaa ya watu wengine. Katika hali hii, mhusika Fumo Liyongo katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* ni mhusika jagina. Kwa upande mwingine Kamusi ya Tuki (2004) inamtaja Jagina kama shujaa na hivyo kumchukua jagina kama mtu mwenye moyo thabiti anayeweza kukabili mambo, hata kama ni hatari. Ni jogoo, nguli, ghazi, batali, jasiri, nyamaume. Aidha utafiti ulibainisha kuwa baadhi ya watunzi wa utenzi hutumia wahusika wasio na sifa za majagina. Kwa mfano mhusika mkuu katika *Utenzi wa Mwana Kupona* hana sifa za kijagina. Hashima ni bintiye Mwana Kupona ambaye ni mhusika mkuu.

Riwaya teule katika utafiti huu zimedhihirisha kuwa na wahusika majagina ambao wamefungamanishwa na matatizo ya kijamii. Matumizi ya wahusika majagina katika riwaya hizi ni taathira ya utenzi kwa ambavyo hata tenzi simulizi ziliwajenga mashujaa wake katika hali ya kuwafungamanisha na matatizo ya kijamii yanayoikabili jamii husika. Utafiti umebainisha kwamba tenzi hizi sawa na riwaya teule zimehusisha wahusika majagina na jamii kwa lengo la kuonyesha kuwa shujaa ni zao la jamii na hana budi kukumbana na matatizo ya wanajamii wengine. Pia hutaka kuwaonyesha wanajamii ushujaa wa shujaa katika kukabiliana na matatizo tofauti tofauti katia jamii.

Aidha, hulenga kuwaondolea wanajamii hofu na kuwahakikishia usalama wao pindi wapatao matatizo. Athari hii inatokana na ukweli wa nadharia ya usemezo kuwa katika usemezo kuna kani kitovu na kani pewa. Katika muktadha huu, kani kitovu ni utenzi ambao uliathiri riwaya teule ambayo ni kani pewa.

Mhusika Dzombo katika riwaya ya *Walenisi* ni kielelezo cha athari ya wahusika jagina wa utenzi katika riwaya teule. Dzombo ni kiumbe wa ukweli ambaye amekuzwa na kujikuza mwenyewe hata akaonekana kiumbe wa ajabu. Riwaya inapoanza tunaona Dzombo akiwa amehukumiwa kifo kwa tuhuma za uchochezi wa jamii yake dhidi ya utawala. Kifo hicho kilikuwa kitekelezwe kwa sayari. Hata hivyo tunaona jagina huyu akishika usukani katika sayari kwa ujuzi wa kufuata maagizo na kufaulu kufika katika nchi ya Walenisi salama hata baada ya kupata changamoto nyingi safarini. Aidha tunafahamishwa kuwa kila mwanajamii alijua kwamba, Dzombo kuingia kwa sayari ni mwisho wa maisha yake. Hali ya kukiepuka kifo inamdhihirisha Dzombo kama jagina.

Tunaona baada ya Dzombo kutembea nchi ya Walenisi na kuona jinsi imeendelea, na kubainisha sababu ya maendeleo hayo kuwa ni mapinduzi, Dzombo anaamua kurudi duniani ili kuwahamasisha wakaazi wa duniani kuhusu harakati za mapinduzi. Moja kwa moja Dzombo anaanza kuwakabili vyongozi wadhalimu kule duniani ili kuwakomboa wanajamii. Tunaona akikabili serikali kwa maneno makali baada ya kwenda kudai malipo ya mimea aliyoagizwa apande na kuelezwa kuwa serikali ndiyo inamdai. Dzombo anaendeleza vuguvugu la kuondoa udhalimu ili kutaifisha mali yote na kuleta ujamaa.

Dzombo ni mhusika mkuu katika riwaya ya *Walenisi*. Kwa mujibu wa Gathara (2013) aghalabu jagina katika utenzi huwa mhusika mkuu. Kwa hivyo matumizi ya Dzombo katika riwaya ya Walenisi yanaenda sambamba na mhusika Fumo Liyongo ambaye ndiye jagina katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Tunaona Fumo Liyongo anapokuwa maarufu miongoni mwa Wagalla, mfalme wa Pate Daudi Mringwari anatiwa kiwewe kwa hofu kuwa heunda Liyongo akampokonya uongozi. Hali hii inapelekea mfalme Mringwari kumwekea Liyongo mitego ili aweze kumuua. Tunaona Liyongo akifaulu kukwepa mitego hii kwa njia ya ushujaa na hatimaye kusalitiwa na mwanaye wa kipekee ambaye alimuua.

Mutiso (1999) anabainisha kuwa majagina wa utenzi waliwekewa mitego na viongozi wao kwa nia ya kuwaangamiza jinsi imejitokeza katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Hali hii inajitokeza katika riwaya teule ya *Walenisi*. Chambilecho nadharia ya usemezo, matini huathiriana. Tunaona Dzombo kama jagina anapojaribu kuwazindua wanajamii kule duniani anatumia kwa uchochezi na hivyo kuhukumiwa kifo. Kwa hivyo anaingizwa katika sayari ili akutane na hatima yake. Hata hivyo anaepuka mtego huu na kusafiri hadi Walenisi. Utafiti ulibainisha kuwa haja ya mtego huu ilikuwa ni kumnyamazisha na kumuangamiza ili viongozi watawala wa duniani waendeleze udhalimu wao.

Katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, Vuai na Marijan wanajitokeza kama wahusika majagina wa jamii. Tunaona vijana hawa kwa ujasiri wao na wafanyikazi wengine wanapanga na kuondoa uongozi wa umwinyi katika jamii yao.

Vuai akiwa mfanyikazi katika shamba la Fuad anajitolea kuhudhuria mikutano ya wafanyikazi kinyume na mwajiri wake. Anaendelea kuhudhuria huku akiwazindua wafanyikazi wenzake kuhusu udhalimu wa wamwinyi na mabwana na jinsi ya kukabiliana nao. Hali hii inapelekea Vuai kufutwa kazi katika shamba la Fuad. Hata hivyo, jagina huyu hakufa moyo kwani aliungana na Marijan na wafanyikazi wengine ili kuleta mageuzi katika jamii yao. Wakiwa Dambwe, Vuai, Marijan na wafanyikazi wengine wanapanga mapinduzi dhidi ya mabwana wa mashamba. Tunaona wanashirikiana na kupigana na mabwana na walinzi wao na kufaulu kuwashinda. Katika harakati hizi wanapindua uongozi ambapo mali yote ya jamii ilitaifishwa na kuendeleza ujamaa.

Katika harakati za mapinduzi, Vuai anakabiliana na mitego na changamoto nyingi. Tunaona Fuad anapogundua kuwa Vuai huhudhuria mikutano ya wafanyikazi, anamfuta kazi ili kumnyamazisha. Hata hivyo, Vuai hakufa moyo wa kuendelea kuwazindua wafanyikazi katika shamba la Fuad. Changamoto alizopitia Vuai zinaoana na changamoto na mitego walizopitia majagina katika utenzi. Kwa mfano, ili mfalme Mringuari amuangamize shujaa Liyongo, anamuita Pate kwa hila ya kutaka kumuua. Anaposhindwa anaamua kumuoza msichana wa Kigalla ili atumike kumuangamiza. Baada ya kushindwa tunaona hila nyingine kama vile kwenda msituni kutafuta makoma wakitarajia kuwa Liyongo atakapoupanda mkoma huo watamuua kwa mshale lakini wanashindwa.

Utafiti ulibainisha kwamba, suala la wahusika majagina wa utenzi kutumika katika riwaya teule sio jambo geni. Kulingana na Bennet (1990) akifafanua mhimili wa nadharia ya usemezo anasema kuwa riwaya husheheni matumizi ya wahusika majagina ambao usuli wao umo katika utenzi.

Aghalabu katika tenzi, jagina ambaye ni mhusika nguli hujihusisha katika safari ambazo ni hatari, na hukumbana na hali ngumu ambazo humrudisha nyumbani akiwa amekengeushwa na hiyo safari (Vutagwa 2013). Sifa hizi kumhusu jagina wa utenzi zinajisheheni katika riwaya teule ya *Walenisi* na *Kasri ya Mwinyi Fuad*.

Mhusika Dzombo katika riwaya ya *Walenisi* anajihusisha na safari ambayo ni hatari na anakumbana na hali ngumu ambazo zinamfanya arudi nyumbani akiwa amekengeuka. Baada ya Dzombo kuhukumiwa kifo kwa tuhuma ya uchochezi, anaingia sayarini na kuelekea nchi ya Walenisi. Jagina Dzombo anazinduliwa kule Walenisi na hivyo kurudi nyumbani duniani akiwa amekengeuka tayari kuwazindua wakaazi wa duniani ili kuleta ujamaa jinsi ilivyo kule Walenisi.

Aidha katika riwaya teule ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, mhusika Vuai ambaye ni jagina anajitokeza kwa safari hatari akiwa na Marijan. Tunaona akihudhuria mikutano ya wafanyikazi ambayo ilimzindua yeye na wenzake na baadaye kusababisha mageuzi ya uongozi katika jamii yake. Tunaona kupitia jitihada zake na Marijan na wafanyikazi wengine, wafanyikazi kama vile Kijakazi na mkongwe wanajinasua kutoka unyanyasaji wa mabwana kama vile Fuad. Jitihada hizi za Vuai na Marijan zilipelekea wafanyikazi kupindua uongozi wa Kisultan uliokuwa na umwinyi na kuleta uongozi mpya wa ujamaa ambapo mali yote ilitaifishwa.

Safari hizi katika riwaya teule ni sawa na safari ya Fumo Liyongo katika utenzi wa Fumo Liyongo. Tunaona Liyongo akikabiliana na uongozi wa mfalme Mringwari bila uoga wowote. Liyongo anachukua hatua hatari kabisa ya kutaka kuletewa kinu gerezani ili akate minyororo kwa nia ya kujinasua. Tunaona anapoletewa kinu kukata minyororo na kutoroka gerezani. Maelezo haya yanaoana na maoni ya Vutagwa (2013) kuwa jagina wa utenzi sawa na riwaya huwa kiongozi, mpiganaji na matendo yake hujitokeza akiwa safarini. Kwa hivyo utafiti ulibainisha kwamba suala la watunzi wa riwaya teule kutumia wahusika majagina ambao wanahusika katika safari ngumu na hatari na kisha kukengeuka ni athari inayotokana na utenzi.

Wahusika majagina katika utenzi hujitokeza kikamilifu na hoja muhimu ambazo zinaoana na jamii husika. Kwa mujibu wa Finnegan (1970) wahusika hawa hushughulika na maswala yanayoiathiri jamii husika. Utafiti ulibainisha kwamba, sawa na jinsi watunzi wa utenzi walichagua wahusika majagina kushughulikia maswala ya jamii, watunzi wa riwaya teule wamefuata mkondo uo huo.

Katika riwaya ya *Walenisi*, mhusika Dzombo ni mfano wa mhusika ambaye anashughulikia maswala ya jamii. Dzombo anapojaribu kuwaelimisha wanajamii na kuusuta utawala dhalimu, anashikwa na kupelekwa mahakamani ili kuhukumiwa. Katika hali hii anahukumiwa kifo. Hata hivyo anaponyoka kifo kwa tundu la sindano na kurudi duniani ili kuendeleza mageuzi kwa nia ya kuleta maendeleo ya wanajamii duniani ili wawe kama kule Walenisi. Harakati hizi zote za Dzombo zilikuwa ni kupigana kwa manufaa ya wanajamii.

Aidha katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, Vuai na Marijan ni wahusika majagina ambao haja yao ilikuwa ni kupigania jamii yao. Kwa mujibu wa Momanyi (1991) wahusika wa aina hii hutumika na watunzi ili kuzindua jamii na kukejeli uongozi dhalimu. Maelezo haya yanaoana na nadharia ya usemezo kuwa usemezo ni kanivali. Tunaona katika riwaya hii kuwa Vuai na Marijan wanatumiwa na mtunzi kama sauti ya jamii katika kupigana na mabwana. Katika hali hii mtunzi kupitia wahusika hawa majagina anawaonya viongozi wenye tabia ya ubwana kuwa ni vyema kuishi vizuri na watu bila kuwadhulumu kwani watawaliwa wakizinduka huenda wakaleta mapinduzi ambayo yatawafanya kupoteza fahari yao. Kwa hivyo, wahusika hawa ni taathira ya utenzi katika riwaya teule kwa ambavyo inaashiria wahusika majagina wa utenzi kama Fumo Liyongo katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* ambaye alipendwa kutokana na uwezo kupigania jamii yake ya Wagalla dhidi ya maadui wa jamii na mfalme Mringwari ambaye aliongoza kwa udhalimu kama vile kutaka kumuua Liyongo ili aweze kuendeleza uongozi wake.

Aghalabu katika utenzi, majagina ni wa kiume. Pale ambapo ni mwanamke, basi huwa hana sifa pia za kijagina kama vile walizo nazo majagina wa kiume (Gathara 2003). Pia anaeleza kwamba ikiwa ni mwanamke, huwa ametenda tendo moja la kijasiri tu. Utafiti ulibainisha kuwa ujasiri ni sifa moja tu ya kishujaa wala hauwezi kamwe kumfanya mtu kuwa shujaa.

Utafiti ulibainisha kuwa riwaya teule zimeakisi kipengele hiki cha jagina kuwa mwanamume. Katika riwaya ya *Walenisi* tunaona mhusika mkuu ambaye ni jagina aitwaye Dzombo ni wa kiume. Aidha riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* inaendeleza sifa hii kwani Vuai na Marijan ambao ni majagina katika jamii hii ni wa jinsia ya kiume. Hata

hivyo tunaona Mariam na Mkongwe wakionyesha ujasiri kwa kukataa kudhulumiwa kimapenzi na Fuad na hatimaye kuacha kazi ili kujiunga na wenzao kwa nia ya kuendeleza mageuzi. Katika hali hii, tunaweza kusema tu kuwa Mariam na Mkongwe ni jasiri bali sio jagina.

Vile vile utafiti ulibainisha kwamba hali ya jamii kumchukulia mwanamume kuwa jagina inatokana na itikadi ya jamii kuwa mwanamume kwa wakati wowote huwa juu ya mwanamke. Kwa hivyo ukombozi na uongozi ni lazima utokane na mwanamume. Kadhalika, inaaminiwa kuwa duniani katika jamii nyingi mwanamke ni mtu mwoga na dhaifu. Tofauti na mwanamume ambaye husawiriwa kama mtu mstahimilifu mwenye uwezo wa kukabiliana na masuala na mambo magumu katika jamii, kama vile vita. Kwa mujibu wa Gathara (2003), hali hii ndiyo ilisababisha kutokea kwa msemu wa ‘jikaze kiume.’ Hata hivyo, maelezo haya hapa juu hayaonyeshi kuwa mwanamke hawezi kuwa jagina. Ingawa tenzi nyingi za Kiswahili hazijamchora mwanamke kama jagina, riwaya za Kiswahili zimefanya hivyo. Mabadiliko haya yanatokana na kipengele cha nadharia ya usemezo ambayo inauweka utanzu wa riwaya katika kiwango cha kani pewa, yaani riwaya za Kiswahili zimejitokeza katika sura tofauti tofauti na hazifanani ukilinganisha na utenzi ambao uko katika kiwango cha kani kitovu na unachukua sura na muundo mmoja katika utenzi wake.

Kwa upande mwingine, Mutiso (1999) anafafanua kuwa baadhi ya tenzi hutumia wahusika ambapo mhusika mkuu sio jagina. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Mwana Kupona*, Mwana Kupona na Hashima ni wahusika ambapo Hashima ni mhusika mkuu ingawa si jagina. Aina hii ya wahusika inaendelezwa katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* ambapo Julia ambaye ndiye mhusika mkuu si jagina. Ingawa mtunzi anatuonyesha safari

yake ya maisha katika ndoa na Kanda na baadaye waziri Mkurutu, hatupati taswira ya jagina. Mtunzi alitaka tu kupitisha ujumbe wake kuhusu changamoto za ndoa. Kwa hivyo matumizi ya wahusika wa aina hii katika riwaya teule ya *Msimu wa Vipepeo* ni taathira ya wahusika sawa na hawa katika utenzi.

4.3 Kiishilio

Sura hii imetathimini taathira ya wahusika majagina wa utenzi katika riwaya teule. Imebainisha kwamba, matumizi ya wahusika majagina katika riwaya teule ni taathira ya wahusika wa utenzi. Utafiti umebainisha kuwa wahusika Vuai na Marijan katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* na Dzombo katika riwaya teule ya *Walenisini* ni wahusika majagina ambao sifa zao zinaakisi wahusika majagina katika utenzi kama vile Fumo Liyongo katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Aidha, matumizi ya wahusika wa kawaida kama vile Julia, Ndumi, waziri Mkurutu na Kanda katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* ni taathira ya wahusika wa utenzi kama vile Bint Hashima na Mwana Kupona katika *Utenzi wa Mwana Kupona*.

Sura inayofuata ni ya mwisho katika utafiti huu. Sura hii imeshughulikia kufafanua na kutolea maelezo masuala ambayo yanahusu muhtasari, matokeo, changamoto na mapendekezo ya utafiti huu.

SURA YA TANO

5.0 Muhtasari na Matokeo ya Utafiti

5.1. Utangulizi

Sura hii imeshughulikia muhtasari wa utafiti mzima kwanzia sura ya kuanza hadi ya mwisho. Aidha, sura hii imetoa matokeo ya utafiti kupitia ugunduzi mbalimbali ambao umetokana na uchunguzi kuhusu kila lengo la utafiti kwa kuzingatia misingi ya nadharia ya utafiti. Vile vile, sura hii imetoa changamoto katika utafiti huu na mapendekezo ya vipengele na maswala muhimu ambayo yanaweza kuwa kichocheo cha uchunguzi mwingine zaidi kuhusu fasihi ya Kiswahili kwa ujumla.

5.2 Muhtasari

Utafiti huu umechanganua athari ya utenzi katika uandishi wa riwaya teule ya Kiswahili. Malengo ya utafiti huu yalikuwa ni kubainisha namna maudhui ya utenzi yalivyowiana na uandishi wa riwaya teule, kuonyesha namna mtindo wa uandishi wa utenzi anavyowiana na uandishi wa riwaya teule na hatimaye kubainisha namna wahusika wa utenzi wanavyowiana na wale wa riwaya teule. Malengo haya yalichanganuliwa na kufafanuliwa kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya usemezo. Malengo haya ya utafiti yametokelezwa kupitia sura tano za tasnifu hii.

Sura ya kwanza imefafanua msingi wa utafiti huu. Sura hii iliangazia usuli wa utafiti ambao uliwekea msingi utafiti huu kwa kuonyesha nafasi ya utenzi katika kuathiri uandishi wa riwaya teule. Aidha, ilibainisha mtindo, maudhui na wahusika wa utenzi na jinsi sifa hizi za utenzi zinaweza kuathiri riwaya teule. Isitoshe, sura hii imejadili suala la utafiti na sababu ambazo zilisababisha mada hii ya utafiti kuchaguliwa. Pia upeo na

mipaka ya utafiti ilijadiliwa katika sura hii. Vile vile, yaliyoandikwa kuhusu mada hii yamejadiliwa katika sura hii ili kubainisha mchango na nafasi ya kazi za utafiti wa awali ambazo zimetajwa katika utafiti huu.

Sura hii ya kwanza pia imejadili nadharia iliyotumiwa katika kuungoza utafiti huu. Nadharia yenyewe ni ya usemezo, utafiti katika sura hii uliangazia waasisi na waitafaki wa nadharia hii na kubainisha wazi mihimili muhimu ambayo iliufaa utafiti huu. Hali kadhalika, mbinu ya utafiti ya usomaji maktabani ilijadiliwa. Pia sampuli na namna ya kuteua sampuli ilijadiliwa katika sura hii.

Sura ya pili ilichunguza athari ya maudhui ya utenzi katika riwaya teule kwa lengo la kubainisha aina ya maudhui ambayo yalitumika katika utenzi na jinsi yanaendelezwa na waandishi wa riwaya teule. Aidha iliangualia historia ya utenzi na riwaya ili kuonyesha kuwa maudhui haya ya riwaya teule ni taathira ya utenzi.

Sura ya tatu ilijadili athari ya mtindo wa utenzi katika uandishi wa riwaya teule. Mitindo ya usimulizi, uunganifu na matumizi ya taswira katika teule ilijadiliwa ili kubainisha kuwa matumizi ya mitindo hii katika riwaya na waandishi wa riwaya teule yanatokana na athari ya utenzi.

Sura ya nne ilishughulikiwa athari ya wahusika majagina wa utenzi katika riwaya teule. Sura hii ilibainisha sifa kuu za wahusika majagina jinsi zinajitokeza katika kazi za riwaya teule na utenzi kwa nia ya kubainisha kuwa matumizi ya wahusika majagina katika uandishi wa riwaya teule ni taathira ya wahusika majagina katika utenzi.

Hatimaye katika sura ya tano, utafiti uliangalia muhtasari wa kila sura ya utafiti huu na matokeo yake kwa kina. Katika kueleza matokeo, kila lengo la utafiti lilichunguzwa na

kukadiriwa iwapo lilitimizwa. Vile vile sura hii, ilijadili matatizo yaliyoukumba utafiti huu na mapendekezo ya utafiti zaidi.

5.3 Matokeo ya Utafiti

Kutokana na uchanganuzi wa data iliyotokana na riwaya teule ambazo ni *Walenisi*, *Kasri ya Mwinyi Fuad* na *Msimu wa Vipepeo*, imebainika kwamba utenzi una athari kubwa katika uandishi wa riwaya teule. Athari hizi za utenzi kwa uandishi wa riwaya teule zinatokana na kipengele cha nadharia ya usemezo kwamba tanzu husemezana na hivyo kuathiriana. Matokeo ya utafiti huu yamejadiliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti ambayo ni; Kubainisha maudhui ya utenzi yalivyoathiri uandishi wa riwaya teule, kuonyesha mtindo wa uandishi wa utenzi ulivyoathiri uandishi wa riwaya teule na hatimaye kubainisha wahusika wa utenzi walivyoathiri wahusika wa riwaya teule.

Utafiti huu ulibainisha kwamba maudhui ya dini, ndoa na malezi katika riwaya teule ni taathira ya maudhui haya katika utenzi. Waandishi wa riwaya teule wametumia ubunifu wao katika kuendeleza maudhui haya. Watunzi hawa wamechukuwa maudhui ya malezi, ndoa na dini kama msingi wa utunzi wao.

Utafiti uligundua kwamba tenzi nyingi za awali ziliegemea dini ya Kiislamu. Hali hii ilitokana na mhimili wa nadharia ya usemezo ambayo inauweka utenzi katika kitengo cha kani kitovu. Hata hivyo, waandishi wa riwaya teule wameegemea dini ya Kikristo, Kiislamu na dini za asili. Hali hii inaweka riwaya katika kitengo cha kani pewa kwani nadharia ya usemezo inachukulia kuwa katika kitengo hiki cha kani pewa hakuna njia moja ambayo waandishi wa riwaya hutumuia katika utunzi.

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* mwandishi ameangazia dini ya Kikristo na kiasili. Suala la Julia kwenda kanisani kuimba katika kwaya na kuhudhuria madarasa ya Biblia ni jambo la dini ya Kikristo. Hii inatokana na ukweli kuwa ni Wakristo ndio hutumia Biblia. Aidha kisa cha Julia kuamini kwamba mganga ndiye angekuwa suluhu kwa ndoa yake linaleta dhana ya dini asili.

Aidha, katika riwaya ya *Walenisi* tunaona kwamba Dzombo anapoingia anga za juu alikuwa na hisi kuwa ameiacha nyuma Jehanamu na kuingia mbinguni. Katika hali hii Dzombo anakuwa na uoga wa kumkabili mwenyezi Mungu. Utafiti ulibainisha kwamba uoga wa Dzombo kumkabili Mungu unatokana na siku ya kيامa ambapo katika dini inaaminika kwamba mtu anapofariki huenda kwa mwenyezi Mungu ili ahukumiwe. Ilibainika kwamba masuala haya na hukumu yalishamiri sana katika utenzi. Tunaona Kijana Mtu-Tabia akimuuliza Dzombo kuhusu kuwasili kwa mwenyezi Mungu kwa sababu majilio yake yalitabiriwa.

Hata hivyo, utafiti ulibaini kuwa suala la dini kutumiwa kama chombo cha kudhulumu wengine halikujitokeza katika utenzi. Katika riwaya ya *Walenisi*, suala hili limejitokeza. Tunaona Wachuna wakiwafahamisha watawala kwamba kuzaliwa maskini ni majaliwa ya Mungu, na hivyo watawaliwa wangoje faraja yao baada ya kifo. Hili ni dhibitisho la dini kutumiwa katika kudhulumu wengine.

Vile vile sawa na jinsi watunzi wa utenzi walitumia dini hasa kipengele cha maombi, Utafiti umegundua kuwa riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* imeakisi mkondo wa utenzi kuhusu dini. Tunaona wahusika katika riwaya hii wakichukulia maombi kwa mwenyezi Mungu kama jambo muhimu. Tunaeleza katika (uk. 14) kuwa Fuad aliteremka baada ya

maombi ya magharibi. Pia tunamuona Shurwani akimuaga Fuad ili aende kusali. Kwa kuzingatia aina ya maombi kama vile maombi ya magharibi na matumizi ya majina kama vile Bi. Maimuna, utafiti ulibainish kuwa masuala ya dini katika riwaya hii ni ya dini ya Kiislamu.

Utafiti ulibainsiha kwamba utunzi kuhusu maudhui ya dini ulikuwepo katika utenzi kabla ya kuanza kutumiwa katika riwaya. Kwa hivyo, matumizi ya maudhui haya katika riwaya teule ni taathira ya utenzi wa Kiswahili.

Utafiti ulibainisha kwamba watunzi wa riwaya sawa na utenzi wameshughulikia maudhui ya malezi kwa kusawiri malezi bora na malezi duni. Imebainika kwamba malezi ya watoto aghalabu ni jukumu la wazazi. Tenzi nyingi za awali zimechora mwanamke kama mlezi mkuu wa watoto. Aidha malezi katika riwaya teule yamesawirika kupitia wazazi wote yaani wa kike na kiume. Hata hivyo malezi ya mzazi wa kike yametiliwa maanani. Utafiti uligundua kuwa watunzi wengi wa Kiafrika humchora mwanamke kama mlezi mkuu kwa sababu itikadi na tamaduni za jamii ya Kiafrika zinampa mwanamke jukumu la malezi.

Shafi, katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* anayasawiri malezi duni kwa watoto. Tunaona Fuad akitelekezwa na mamake Bi. Maimuna. Fuad anapomwamrisha Kijakazi. Bi. Maimuna anafurahia suala hili badala ya kumwelekeza Fuad. Tunafahamisha kuwa Fuad alikuwa mtoto mtundu ambaye angefanya lolote ikiwemo kupasua vitu ndani ya nyumba na hakuna yeyote aliyeweza kumkanya kwani lolote alilofanya lilikuwa sawa mbele ya wazazi wake.

Utafiti ulibainisha kuwa maisha ya Fuad kwenda kombo baada ya wazazi wake kufariki yalitokana na malezi duni. Tunaona Fuad akijaribu kumnajisi Mariam. Fuad anashindwa hata na kuoa kwa sababu hakuwa na maarifa ya kuongea na watu. Yeye alifikiri tu kuwa uwezo wake wa kuamrisha ungemfaidi kila kitu alichotaka. Hali hii inatokana na msingi wa malezi aliyopewa Fuad. Kwani wazazi wake wakiongozwa na Bi. Maimuna hawakutaka atangamane na watu wengine akiwemo mlezi wake Kijakazi.

Ukilinganisha malezi katika riwaya hii na *Utenzi wa Mwana Kupona*, tunaona kuwa yanahitilafiana. Katika *Utenzi wa Mwana Kupona*, Mwana Kupona ni kiwakilishi cha malezi bora kwani yeye anamwelekeza bintiye jinsi ya kuishi vyema na mumewe na jamii kwa ujumla. Kwa hivyo, uhusiano wa maudhui ya malezi katika utenzi na riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* ni mahusiano ya kani kitovu na kani pewa ambapo kani pewa inajaribu kutenganisha maudhui haya na kani kitovu inajaribu kuoanisha maudhui haya katika utenzi na riwaya teule.

Vile vile riwaya teule ya *Msimu wa Vipepeo* inasawiri maudhui ya malezi. Riwaya hii inaonyesha nafasi ya baba mzazi katika malezi ya mtoto. Tunaona baada ya Julia kutalakiana na Kanda, mtoto wao Ndumi hafurahii maisha ya kukaa na baba wa kambo waziri Mkurutu. Hali hii inapelekea Ndumi kumtafuta babake mzazi bwana Kanda. Utafiti ulibainisha kuwa mtunzi alitunga kisa hiki ili kudhihirisha changamoto ya malezi hasa jamii ya sasa kwani mtunzi huchota malighafi kutoka katika jamii na mazingira yake.

Utafiti uligundua kuwa maudhui ya malezi katika riwaya teule ni taathira ya utenzi kwa ambayo maudhui haya yaliendelezwa kwanzia katika utenzi simulizi kabla ya maandishi.

Maelezo haya yanaoana na kipengele cha nadharia ya usemezo kinachosema kuwa matini ni uwanja ambao ni mwingiliano wa kiusemezo baina ya sauti mbalimbali za usemi. Kila matini hurejelea matini nyinginezo zilizopo za wakati uliopo na za wakati ujao.

Kazi ya fasihi ina sauti mbalimbali zinazoingiliana na kupiga mwangwi katika kazi zingine zilizotangulia. Utafiti ulibaini kuwa matumizi ya maudhui ya ndoa katika riwaya teule ni taathiri ya utenzi. Ndoa ndiyo huendeleza ukuaji wa jamii. Kwa hivyo, ndoa ndiyo msingi wa jamii. Hali hii ndiyo hupelekea watunzi wengi kuangazia suala la ndoa katika jamii. Riwaya teule zimesawiri maudhui haya kupitia ndoa mbalimbali.

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, tunaona ndoa kati ya Kanda na Julia. Ndoa hii inadumu kwa miaka kumi na mitano kisha Julia anamtalaki Kanda kutokana na umasikini. Tunaona Julia anaingia katika ndoa nyingine na waziri Mkurutu ambapo ingawa kuna pesa, inajawa na changamoto nyingi suala linalofanya Julia kutamani ndoa yake na Kanda. Hapa mtunzi alilenga kuonyesha changamoto katika ndoa ambazo zinakumba jamii ya sasa.

Aidha, katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* tunaonyeshwa ndoa baina ya Bw. Malik na Bi. Maimuna ambao walipendana sana. Aidha katika riwaya ya *Walenisi* tunapata ndoa ya Dzombo na Bi. Fikirini kule walenisi. Utafiti ulibainisha kwamba maudhui ya ndoa katika riwaya teule ni taathira ya maudhui ya ndoa katika utenzi.

Pia, utafiti ulipata kwamba kuchunguza historia ya tanzu zinazoathiriana ni muhimu katika usemezo. Hali hii inatokana na mhimili wa nadharia ya usemezo kuwa historia katika usemezo husaidia kuelewa maana na kufaidika na kazi za kifasihi.

Kuhusu mtindo, utafiti ulibaini kuwa ubunifu wa mtunzi hubainika kupitia uchunguzi wa mtindo ambao umetumiwa na mtunzi katika kazi husika ya fasihi. Mtunzi hutumia mtindo fulani kwa madhumuni ya kupitisha ujumbe. Utafiti ulibainisha kwamba matumizi ya mtindo wa usimulizi, uunganifu na taswira katika riwaya teule haukuzuka hivi hivi, bali unatokana na matumizi ya mitindo hizi katika utenzi.

Utafiti uligundua kuwa riwaya teule sawa na utenzi zimetumia masimulizi ya kihistoria, sira na safari. Masimuli haya ndiyo yamejenga msuko wa riwaya teule.

Riwaya teule ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* ni mfano ambao mtunzi ametumia masimulizi ya kihistoria. Kupitia masimulizi haya ya shamba la Fuad, mtunzi anatusimulia jinsi tabaka la wafanyikazi lilipigana na mabwana na wakoloni ili kuleta ujamaa. Kupitia masimulizi haya tunapata mwanga kuhusu maana ya ujamaa na chanzo chake katika kisiwa cha Zanzibar.

Aidha, katika riwaya hii ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, mtunzi anatusimulia kuhusu maisha ya Fuad. Utafiti ulibainisha kuwa haya ni masimulizi ya sira kwani mtunzi ameyaeleza maisha ya Fuad tangu akiwa mtoto, malezi yake hadi alivyokuwa mtu mzima. Mbali na *Utenzi wa Fumo Liyongo* kutumia masimulizi ya kihistoria pia umetumia masimulizi ya sira kwa sababu tunasimuliwa maisha ya Fumo Liyongo kuanzia utotoni, utu uzima hadi kuaga kwake. Kwa hivyo, matumizi ya mtindo huu wa masimulizi katika riwaya ni taathira ya utenzi.

Vile vile riwaya ya *Walenisi* imetumia mtindo wa masimulizi. Mtunzi anatuonyesha kupitia masimulizi ya safari jinsi Dzombo alisafiri hadi nchi ya Walenisi na kuzinduliwa kule kuhusu maendeleo ya walenisi yaliyotokana na ujamaa. Mtunzi anatusimulia tena

safari ya Dzombo kutoka Walenisi hadi duniani ili kuleta uzinduzi kwa wanajamii kwa nia ya kuleta ujamaa ambao ungeleta maendeleo.

Utafiti ulibaini kwamba mtindo wa masimulizi ulikuwa mtindo wa kipekee katika utunzi wa utenzi. Hata hivyo watunzi wa riwaya wamechota mtindo huu kutoka kwa utenzi na kuuendeleza katika riwaya teule. Kwa hivyo, matini ya mtindo wa masimulizi ya utenzi yametumika kama malighafi katika riwaya teule.

Ilibainika kwamba msuko na mfuatano wa visa katika riwaya teule umepangwa kimantiki. Mtindo huu unaitwa uunganifu. Utenzi wa Kiswahili una sifa hizi za kuwa na msuko wa kimantiki. Utafiti ulibainisha kuwa riwaya teule zina uunganifu na mtiririko wa visa vyenye mantiki.

Uunganifu katika riwaya ya Kasri ya Mwinyi Fuad inajitokeza kwa kuwepo mtiririko wa matukio ambayo yamepangwa katika sura tatu ndefu. Riwaya hii imejengwa kwenye msingi wa familia ya Bw. Malik na Bi. Maimuna ambao ni wazazi wa Fuad. Tunafahamishwa jinsi Fuad alilelewa baada ya wazazi wake kufa. Mtunzi anatuonyesha mateso waliyopitia wafanyikazi katika shamba la Fuad. Mateso haya yanasababisha wafanyikazi kujiunga pamoja na kuupindua uongozi wa masultan. Katika harakati hii Fuad anapoteza mali yake kwa wafanyikazi kutokana na kutaifishwa kwa mali yote na kuleta ujamaa.

Aidha mtindo wa uunganifu unajitokeza katika riwaya ya *Walenisi* pale ambapo Dzombo anahukumiwa kwa tuhuma za uchochezi, safari yake hadi nchi ya Walenisi na hatimaye kurudi duniani.

Utafiti ulipata kwamba mtindo wa uunganifu katika riwaya ni taathira ya utenzi. Mtindo huu umeendelezwa na watunzi wa riwaya teule kutoka katika utenzi. Kwa hivyo mwingiliano matini ni uzalishaji wa maana ndani ya matini bali sio ndani ya mahusiano.

Taswira ni maelezo yanayojenga picha, jambo au hali akilini mwa msikilizaji au msomaji (Wamitila 2003). Utafiti ulibainisha kwamba taswira katika utenzi sawa na riwaya humsaidia msomaji katika kuelewa mazingira au mandhari na vitu vinavyoonekana. Katika hali hii, msanii hutilia msisitizo na mkazo kauli ambazo zimeshatolewa. Chambilecho nadharia iliyouongoza utafiti huu hakuna usemi ambao mtu anaweza kuutoa na aseme yeye ni wa kwanza kufanya hivyo. Ilibainika kwamba kila anayesema jambo huwa anatarajia jibu. Hivyo watunzi wa riwaya teule wamechora taswira fulani ili watu wapate funzo na wajiepushe na lile lenye kuleta hasara.

Riwaya teule ya *Walenisi* ni mfano mzuri wa mtunzi kutumia mtindo wa taswira. Mkangi anatupa taswira kamili ya duniani na kule Walenisi. Mtunzi anafananisha duniani na Jehanamu katika hali hii mtunzi analenga msomaji kupata picha kamili ya mateso yanayopatikana duniani. Aidha anafananisha nchi ya Walenisi na mbinguni. Katika hali hii anatupa picha ya Walenisi kama nchi huru. Riwaya teule za *Kasri ya Mwinyi Fuad* na *Msimu wa Vipepeo* zimeakisi mtindo huu. Utafiti ulibainisha kwamba matumizi ya mtindo wa taswira katika riwaya teule yanatokana na watunzi wa riwaya hizi kuathirika na utenzi.

Kuhusu wahusika, utafiti ulibainisha kwamba matumizi ya wahusika majagina katika riwaya teule ni taathira ya wahusika wa utenzi. Ilibainika kwamba wahusika Vuai na Marijan katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* na mhusika Dzombo katika riwaya ya

Walenisi ni wahusika majagina ambao sifa zao zinaakisi wahusika majagina katika utenzi.

Aidha, utafiti pia ulipata kwamba baadhi ya tenzi kama vile *Utenzi wa Mwana Kupona* hutumia wahusika ambao sio majagina. Kwa hivyo, matumizi ya wahusika kama vile Julia, Kanda na waziri Mkurutu katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* inatokana na athari ya utenzi kwa mtunzi wa riwaya hii.

5.4 Changamoto

Utafiti huu ulikumbwa na changamoto kadha. Kulikuwa na changamoto ya kutofautisha kati ya sifa za kimtindo na za kimuundo za utenzi wa Kiswahili. Hata hivyo tafiti za awali ziliusaidia utafiti kupata mwelekeo na kubainisha sifa za kimtindo. Aidha, baadhi ya data kutoka kwa riwaya teule iliingiliana sana kiasi kwamba maelezo yale yale ya kipengele kutoka riwaya moja yangejitokeza tena kueleza kipengele tofauti.

5.5. Mapendekezo

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza athari ya utenzi katika uandishi wa riwaya teule. Utafiti ulionyesha jinsi maudhui, mtindo na matumizi ya wahusika majagina katika riwaya ni taathira ya utenzi. Mbali na kuchunguza haya yote, kuna haja ya kufanya utafiti zaidi ili kubainisha taathira ya utenzi katika tanzu nyingine kama vile hadithi fupi na tamthilia

Aidha, kutokana na umuhimu wa lugha katika utunzi, itafaa utafiti zaidi ufanywe ili kubainisha taathira ya lugha ya ama utenzi au ushairi katika tanzu zingine za fasihi ya Kiswahili.

MAREJELEO

- Anaye, J. (2004). “ *Hadithi kama Chombo cha Maudhui Katika Fasihi; Uchanganuzi wa Riwaya za Mkangi, Mafuta (1984), na Walenisi (1995).*” Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Bakhtin, M. (1978). *The Formal Method in Literary Scholarship*; London, John Hopkins University Press.
- Bakhtin, M. (1981). *The Dialogic Imagination: Four Essays*. Austin; University of Texas Press.
- Bennet, T. (1990). *Outside Literature*. London. Routledge.
- Dalbak, E. (2003). “ *From The Epic To The Novel; A comparative study of Beowulf and Grendel.*” Tasnifu ya uzamifu, Middle East Technical University. (Haijachapishwa)
- Finnegan, R. (1970). *Oral Literature In Africa*. Nairobi: Oxford University Press.
- Fokkema, D. et al (1979). *Theories of Literature in the 20th century*, London: Hurst and Co. Ltd.
- Gathara, K. (2003). *Taswira ya Jagina Katika Tendi: Ulinganisho wa Nabii Isa na Fumo Liyongo. Tasnifu ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Gichamba, J. (2005). *Sifa za Mashujaa na Umuhimu wao kwa Jamii Zao: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu*. Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Holiquist, M. (1990). *Dialogism; Bakhtin and His World*, London. Routledge.
- Hoogvelt, M. (1976). *The Sociology of Developing Societies*. London: Macmillan.

- Kahara , J. (2011). *Tamthilia Kama Utendi; Uchanganuzi Linganishi WA Tamthilia Za Kinjeketile na Mzalendo Kimathi*, Tasnifu Ya Uzamifu, Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Kamau, M. (1992). “Ufundi Katika Riwaya za Mohammed Said Abdulla” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Karama, R. (1996). “*Al-Inkishafi; Ushahidi Wa Usemezo Katika Ushairi Wa Kiswahili.*” Tasnifu Ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Kea, P. (2006). “*Usemezo Katika Nyimbo Za Taarab.*” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachaishwa)
- King' ei, K. na Kemoli, A. (2001) *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.
- Kristeva, J. (1980). *Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature Art*. New York: Colombia University Press.
- Maitaria, J. (2012). “*Uainishaji Wa Ushairi Wa Kiswahili; Dhima Ya Methali.*” Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Masinde, E. (2003). '*Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui*'. Tasnifu ya Ph.D. Nairobi, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)
- Mberia, (1989). “Fumo Liyongo.” Katika. *Mulika Proc.7th SR-CRSP workshop, ILRAD, Nairobi, Kenya. 27th to 28th Feb, 1989*. Vaccine 26:2788- 2795;
- Mkangi, G. (1995). *Walenisi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mohammed, B. (2008). “*Masemezano Kama Mkakati Wa Kufahamu Riwaya za Babu Alipofufuka (2001). Bina-adamu(2002) na Mkusanyiko wa Hadithi Fupi Wa*

- Sadiki Ukipenda*(2000.” Tasnifu Ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta.
(Haijachaishwa)
- Mohamed S.A. (1995). *Kungu za Nadharia za Kiswahili: Tamthilia, Riwaya na Hadithi Fupi*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.
- Momanyi, C. (1991). “*Matumizi ya Taswira kama Kielelezo cha Uhalisi katika utenzi wa Al- Inkshafi*.” Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. East Africa Educational Publishers.
- Madumulla, J. (2009). *Riwaya ya Kiswahili, Historian a Misingi ya Uchambuzi*. Nairobi: Sitima Printer and Stations L.t.d.
- Mulokozi, M. (1989). *Tanzu Za Fasihi Simulizi*; Mulika : Dar es salaam.TUKI.
- Mulokozi, M. (1996). *Utangulizi Wa Fasihi Simulizi*: Dar es Salaam; TUKI.
- Mulokozi, M. (1999). *Tenzi Tatu Za Kale*. Dar es Salaam; TUKI.
- Mulokozi, M. (2002). *The African Epic Controversy: Historical, Phylosophycal and Aesthetic. Perspectives on Epic and Performance*. Dar es Salaam. Mkuki na Nyota
- Mukarovsky, J. (1977). *The World and the Verbal Art; Selected Essays*. New Haven. Yale University Press.
- Muriithi, J. (2002). “*Usemazano katika Tamthilia ya Kiswahili*.” Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Mutiso, K. (1985). *Sira ya Majagina Buddha na Muhammed*. Beyreuth: Swahili Kollaquim University

- Ndumbaro, E. (2013). *Shujaa wa Tendi na Matatizo ya Kijamii*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Ndungo, C. (1985) '*Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria Katika Fasihi ya Kiswahili*.' Tasnifu ya M.A. Nairobi.Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Njogu, K. na R. Chimera. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu: Jomo Kenyatta Foundation*.
- Njogu, K. (2004). *Reading Poetry As Dialogue*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation
- Njogu, K. (1993). "*Dialogic Poetry; A Contestation and Social Challenge in East Africa Poetic Genres*" PHD Thesis. Yale University.
- Omutimba, C. (2015). "*Usimulizi Katika Riwaya Za; Adili na Nduguze, Walenisi, Babu Alipofufuka.*" Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Senkoro, F. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam. Press and Publicity Centre
- Senkoro, F. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha na Fasihi*. Dar es Salaam: KUTTU.
- Shafi, A. (2007). *Kasri ya Mwinyi Fuadi*. Nairobi; Vide Muwa Publishers.
- Swaleh, A. (1992). "*Maudhui Katika Utenzi wa Mwanakupona*". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi:(Haijachapishwa)
- Vutagwa, F. (2013). "*Sifa Za Kiuhalisiaajabu na Umuhimu Wake katika Utenzi wa Mwana Fatuma.*" Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Wafula, R. na N. Kimani (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wafula, R. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia, Historia na Maendeleo yake*. Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. (2002). *Kichocheo cha Fasihi*. Nairobi, Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Misingi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Ltd.

Wamitila, K. (2006). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*, Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. (2006). “*Msimu wa Vipepeo*, Nairobi: Vide Muwa Publishers Ltd.

Wanyela, J. (2013) *Matumizi ya Ushairi Katika Tamthilia Za Kiswahili.*” Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Wellek, R. na A. Warren. (1949) *Theory of Literature*. Harmondsworth: Penguin Books Ltd.

KIAMBATISHO A

Utenzi wa Mwana Kupona (Mulokozi, M. 1999)

1. Negema wangu binti,
Mchachefu wasanati,
Upulike wasiyati,
Saa ukazingatiya.

2. Maradhi yamenishika,
Hata yametimu mwaka,
Siyapata kutamka,
Neno lema kukwambiya.

3. Ndoo mbe ujilisi,
Na wino na qaratasi,
Moyoni nina hadithi,
Nimependa kukwambiya.

4. Kwisakwe kutaqarabu,
Bismillahi kutubu,
Umtaye na Habibu,
Na sahabaze pamoya.

5. Ukisa kulitangaza,
Ina la Mola Muweza,
Basi tuombe majaza,
Mungu tatuwafikiya.

6. Mwanadamu si kitu,
Na ulimwengu si wetu,
Walau hakuna mtu,

Ambaye atasaliya.

7. Mwanangu twaa waadhi,
Pamoya na yangu radhi,
Mungu atakuhifadhi,
Akuepue na baa.
8. Twaa nikupe hirizi,
Uifungeto kwa uzi,
Uipe na taazizi,
Upate kuyangaliya.
9. Nikutungie kidani,
Cha lulu na marijani,
Nikuvike mke shani,
Shingoni kikizagaa.
10. Penda nikupe kifungo,
Kizuri kisicho ongo,
Uvae katika shingo,
Utaona manufaa.
11. Yangu utakaposhika,
Mwanangu hutosumbuka,
Duniani utavuka,
Na Akhira utakiya.
12. La kwanda kamata dini,
Faradhi usiikhini,
Na sunna ikimkini,
Na wajibu kuutiya.

13. Pili kuwa na adabu,
Na ulimi wa thawabu,
Uwe kitu mahabubu,
Kula utakapongiya.
14. La tatu uwe sadiqi,
Ushikalo ulithiqi,
Mtu asoshika haqi,
Sandamane naye ndiya.
15. Tena mwanangu idhili,
Mbee za maqabaili,
Uwaonapo mahali,
Angusa kuwenukiya.
16. Wangiapo wenukie,
Na moyo ufurahie,
Kisa uwapeke mbee,
Watokapo kwenda ndiya.
17. Ifanye mteshiteshi,
Kwa maneno yaso ghashi,
Wala sifanye ubishi,
Watu wakayatukiya.
18. Nena nao kwa mzaha,
Yaweteyao furaha,
Yawapo ya ikraha,
Kheri kuinyamaliya.

19. Wala situkue dhana,
Kwa mambo usoyaona,
Na kwamba na kunong'ona,
Tahadhari nakwambiya.
20. Sitangane na watumwa,
Illa mwinda wa khuduma,
Watakuvutia tama,
La-buda nimekwambiya.
21. Sandamane na wainga,
Wasoyuwa kuitunga,
Ziumbe wasiyo tanga,
Wata kuwaqurubiya.
22. Mama pulika maneno,
Kiumbe ni radhi tano,
Ndipo apate usono,
Wa Akhira na duniya.
23. Nda Mungu na Mtumewe,
Baba na mama wayuwe,
Na ya tano nda mumewe,
Mno imekaririwa.
24. Naawe radha mumeo,
Siku zote mukaaao,
Siku mukhitariwao,
Awe radhi mekuwiya.

25. Na ufapo wewe mbee,
Radhi yake izengee,
Wende uitukuzie,
Ndipo upatapo ndiya.

26. Siku ufufuliwao,
Nadhari nda mumeo,
Taulizwa atakao,
Ndilo takalotendewa.

27. Kipenda wende peponi,
Utapekwa dalihini,
Kinena wende motoni,
Huna budi utatiwa.

28. Keti nae kwa adabu,
Usimtie ghadhabu,
Akinena simjibu,
Itahidi kunyamaa.

29. Enda nae kwa imani,
Atakalo simkhini,
We nae sikindaneni,
Mkindani huumiya.

30. Kitoka agana naye,
Kingia mkongowee,
Kisa umtandikie,
Mahala pa kupumuwa.

31. Kilala si' ikukuse,

Mwegeme umpapase,
Na upepo nasikose,
Mtu wa kumpepeya.

32. Kivukia simondowe,
Wala sinene kwa yowe,
Keti papo siinuwe,
Chamka kakuzengeya.

33. Chamka si' imuhuli,
Mwandikie ma' akuli,
Na kumtunda muili,
Kumsinga na kumwowa.

34. Mnyowe umpalize,
Sharafa umtengeze,
Na udi mfukize,
Bukurata wa ashiya.

35. Mtunde kama kijana,
Asiyeyuwa kunena,
Kitu changalie sana,
Kitokacho na kungiya.

36. Mpumbaze apumbae,
Amrie sikatae,
Maovu kieta yeye,
Mungu atakuteteya.

37. Mwanagu siwe mkoo,
Tenda kama uonao,

Kupea na kosha choo,
Sidharau mara moya.

38. Na koa na kuisinga,
Na nyee zako kufunga,
Na yasimini kutunga,
Na firashani kutiya.

39. Nawe ipambe libasi,
Ukae kama harusi,
Maguu tia kugesu,
Na mikononi makowa.

40. Na kidani na kifungo,
Sitoe katika shingo,
Muili siwate mwengo,
Kwa marashi na daliya.

41. Pete sikose zandani,
Hina sikome nyaoni,
Wanda siwate matoni,
Na nshini kuitiya.

42. Nyumba yako inadhifu,
Mumeo umsharifu,
Wakutanapo sufufu,
Msifu ukimtaya.

43. Muyuwe alipendalo,
Nawe lifuate lilo,

Yambo limtukialo,
Siwe mwenye kumweteya.

44. Utukiwapo kutoka,
Sharuti ruhusa taka,
Uonapo meudhika,
Rudi na kuiketiya.

45. Fuwata yake idhini,
Awe radhi kwa yaki,
Wala sikae ndiani,
Saa ya 'ne ikasiya.

46. Wala sinene ndiani,
Sifunue shiraani,
Mato angalia tini,
Na uso utie haya.

47. Rejea upesi kwako,
Ukae na mume wako,
Utengeneze matandiko,
Mupate kuilalia.

48. Mume wako mtukuze,
Sifa zake zieneze,
Wala simsharutize,
Asichoweza kutoa.

49. Akupacho mpokee,
Na moyo ufurahie,
Asolitenda kwa yeye,

Huna haja kumwambia.

50. Uonapo uso wake,

Funua meno uteke,
Akwambialo lishike,
Illa kuasi jalia.

51. Mama sinue ulimi,

Nioleza wako umi,
Nalioa nyaka kumi,
Tusitete siku moya.

52. Alinioa babako,

Kwa furaha na ziteko,
Tusondoleane mbeko,
Siku zote twalokaa.

53. Siku moya tusitete,

Ovu langu asipate,
Na lake nisilikute,
Hata akakhitariwa.

54. Yalipokuya faradhi,

Kanikariria radhi,
Nkashukuru nkafawidhi,
Moyo wangu nikatoshea.

55. Tangu hapo hata yeo,

Siyanyamaa kilio,
Nikumbukapo pumbao,

Na wingi wa mazoea.

56. Watu wikipulikana,

Milele hukumbukana,

Ila wenye kushindana,

Daima huiyutia.

57. Mausiyo ya mvuli,

Allah allah yaamini,

Na nduguzo na ahali,

Wapende nakuusiya.

58. Uwaonapo sahibu,

Ambao wakusanibu,

Wakikwambia karibu,

Angusa kukurubia.

59. Na wachandika chakula,

Uchambiwa nawe nla,

Wala siweke muhula,

Nyuma nyuma kurejeya.

60. Wala sifanye kiburi,

Nla hata ushakiri,

Usiyakuta siqiri,

Ukambwa na kondolewa.

61. Watu wote waumini,

Kwako na wawe wendani,

Sipende masalatini,

Washinde ukiwapuwa.

62. Sipende wenye jamali,
Na utukufu wa mali,
Fuqara ukawadhili,
Cheo ukamvundiya.

63. Akupendae mpende,
Akuizao mwenende,
Kwa zema mvundevunde,
La' ala akaridhiya.

64. Na ayapo muhitaji,
Mama kwako simuhuji,
Kwa uwezalo mbuji,
Angusa kumtendeya.

65. Mama haya yasikize,
Tafadhali sinipuze,
Utaona nafuuze,
Za akhira na duniya.

66. Tamati maneno yangu,
Kukuusia mwanangu,
Sasa tumuombe mungu,
Anipokelee dua.

67. Kwani yote tunenao,
Mwanaadamu ni puo,
Mola ndiye awezao,
Kupoteza na kongowa.

68. Nakuambawe manani,
Unitilie auni,
Ninenayo ulimini,
Na yote nisoyatowa.

69. Yote nimezoyanena,
Rabi taqabali minna,
Na yasaliyeo tena,
Rabi mola nitendeya.

70. Niwekea wangu wana,
Na umbu langu mnuna,
Yakue yao maina,
Yenee majimbo piya.

71. Rabi waweke nduzangu,
Na wana wao na wangu,
Wenee na ulimwengu,
Kwa jamali na sitawa.

72. Na jamii islamu,
Mola wangu warahamu,
Matakwa yao yatimu,
Nyoyo zikifurahiya.

73. Ya allahu wangu bwana,
Nimekupa ni amana,
Watunde mola rabana,
Siwate kuwa' ngaliya.

74. Nimekupa duniani,
Watunde uwahizini,
Unipe kesho peponi,
Mbee za tumwa nabija.
75. Wangalie kwa huruma,
Uwongoze ndia njema,
Wapulie na tama,
Za akhira na duniya.
76. Kwako kuomba sikomi,
Wala sifungi ulimi,
Ya mufarijal'hami,
Nikomesheze udhiya.
77. Nisimeme muhitaji,
Mjao nakutaraji,
Ajili bi'faraji,
Ya afuwa na afiya.
78. Nondolea ndwee mbovu,
Yaloningia kwa nguvu,
Dhambi zangu na maovu,
Ya rabi nighufiriya.
79. Kwetu yangawa mazito,
Kwako wewe ni matoto,
Nepulia uvukuto,
Unepuke mara moya.
80. Nakuombawe latifu,

Unondolee mikhafu,
Kwa yaumu-li-arafu,
Na idi ya udhuniya.

81. Kwa siku hizi tukufu,
Za kuhiji na kutufu,
Niafu rabi niafu,
Unishushize afuwa.

82. Ya allahu ya allahu,
Ya rabahu ya rabahu,
Ya ghayatu raghbatahu,
Nitika hukwamkuwa.

83. Nakuombawe rabbana,
Bi asmaika 'lhusuna,
Tisia wa tisiina,
Mia kupungua moya.

84. Nipulishie walimu,
Wakinena yafahamu,
Dua hini isilamu,
Akiomba hujibiwa.

85. Nami mjao dhaifu,
Mwenye nyingi takilifu,
Nakuomba takhafifu,
Rabi nitakhafifya.

86. Nakuomba taisiri,
Mambo nisiyakadiri,

Unegeshe kulla kheri,
Shari ukinepuliya.

87. Ya rabi nitimiliza,
Mambo nisiyoyaweza,
Wala moyoni kuwaza,
Kwamba yatasikiliya.

88. Rabi unifurahishe,
Mambo mema unigeshe,
Maovu uyagurishe,
Tusikutane pamoya.

89. Uniweke duniani,
Miongo ya wahusuni,
Nifapo nende peponi,
Makao ya hifadhiya.

90. Ntungile utungo hunu,
Kwa zakumu na zitunu,
Kwa kadha yako dayanu,
Na hukumuzo jaliya.

91. Ntungile nilisaqimu,
Moyo usi na fahamu,
Usomeni islamu,
Mukiongozana ndiya.

92. Na sababu ya kutunga,
Ni shairi si malenga,

Nina kijana muinga,
Napenda kumuusiya.

93. K'apenda kumnabihi,
La'ala katanabahi,
Kamfuata ilahi,
Pamwe na wake rijaa.

94. Somani nyute huramu,
Maana muyafamu,
Musitukue laumu,
Mbee za mola jaliya.

95. Somani mite ya nganu,
Mutii waume wenu,
Musipatwe na zitunu,
Za akhira na duniya.

96. Mwenye kutwii mvuli,
Ndake jaha na jamali,
Kulla endapo mahali,
Hutangaa yake ndia.

97. Mwenye kutunga nudhumu,
Ni gharibu mwenye hamu,
Na ubora wa ithimu
Rabi tamghufiriya.

98. Ina lake mufahamu,
Ni mtaraji karimu,

Mwana kupona mshamu,
Pate alikozaliwa.

99. Tarakhiye kwa yakini,
Alifu wa miateni,
Khamsa wa sabini,
Hizi zote hijiriya.

100. Na baitize idadi,
Ni miati maadudi,
Na mbili za mazidadi,
Ndiyo zimezozidiya.

101. Mola tatusahiliya,
Kwa baraka za nabiya,
Na maswahaba pamoya,
Dini walioteteya.

102. Nahimidi kisaliya,
Kwa tume wetu nabiya,
Ali zake na dhuriya,
Itwenee sute piya.

KIAMBATISHO B

Utenzi wa Fumo Liyongo (Mulokozi, M. 1999)

1. Unipe wimo mweusi
Na ya shamu karatasi
Na kalamu ya unyasi
Unipe kuyandikiya
2. Unipe wimo mweusi
Na ya shamu karatasi
Na kalamu ya unyasi
Unipe kuyandikiya
3. Na kibao cha fakhari
Mpijie misitari
Kwati zende kwa uzuri
Zifuwate moyo ndiye
4. Hadithi na niwandikiye
Ya ajabu musikiye
Yalojiri amjriye
Mupate kufahamiya
5. Niweleze kwa utungo
Hadithi ya liyongo
Niweleze na mazingo
Mambao yalomzingiya
6. Liyongo kitakamali
Akabalighu rijali
Akawa mtu wa kweli
Na haiba kaongeya

7. Kimo kawa mtukufu
Mpana sina mrefu
Majimboni yu marufu
Watu huya kwangaliya
8. Walienenda wagala
Kwa jumbe wa pate dola
Kwa kununua chakula
Pamoya kumwangaliya
9. Wagala hao yuwani
Ni wakuu wa mwituni
Kabla ya sulutwani
Mashujaa wot'e piya.
10. Sulutwani pate bwana
Papo naye akanena
Wagala mumemuona
Liyongo kiwatokeya?"
11. Wagala wakabaini
"Huyu liyongo ni nyani
Kwetu hayusilikani
Wala hatuyasikiya"
12. Mfalme kawambiya
Wagala kiwasifiya
"huwegema watu miya
Wasiweze hukimbiya.
13. "Ni mwanamume swahihi
Kama samba una zihi

- Usiku na asubuhi
Kutembea ni mamoya
14. Ghafula kikutokeya
Mkoyo hukupoteya
Tapo likakuwiliya
Ukatapa na kuliya
15. Mato kikukodoleya
Ghafula utazimiya
Kufa kutakurubiya
Kwa khaufu kukungiya
16. Wagala wakupulika
Kwa dhihaka wakateka
Wakanena”twamtaka
Na sisi kumwangaliya”
17. Na yeye ali kiketi
Kwa nduze wasi katiti
I huko yake baiti
Kwa mwaungwana masha
18. Mfalume kaandika
Waraka wake haraka
Mtu wake kampeka
Liyongo kampekeya
19. Piya akamwandikiya
Wakala walomwambiya
“ndoo nimekuusiya
Wataka kukangaliya”

20. Tumi kenda kwa haraka
Kwa liyongo akafika
Kampa kaumunika
Akasoma yot'e piya
21. Na liyongo akajibu
Kwa hishima na adabu
“ nitakuja kwa karibu
Nitwiiye maulaya”
22. Kisa tumi akarudi
Hata kwa wake sayyidi
Salamu kairadidi
Liyongo mezomwambiya
23. Liyongo siku ya pili
Ndiya akaikabili
Kainenda tasihili
Ndiya akaiemeya
24. Kaifunga kwa sitawa
silaha za kuteuwa
panda tatu katukuwa
kasiwangaa pamoya
25. Na mtu kitoka shaka
Hata pate ukafika
Siku nne kwa haraka
Alo hodari sikiya
26. Liyongo akikabili
Ndiya kenenda rijali

- Alikwenda siku mbili
Na ya pili ni kungiya
27. Liyongo kenda muini
Akipata mlangoni
Panda katia kanwani
Kivuzia kapasuawa
28. Kiivuzia hakika
Muini wakashituka
Panda ikapasuka
Wagala wakasikiya
29. Wakauliza ‘N’
nini vuwi melipija nani?
Akajibu sulutwani.
“Ni liyongo amekuya.”
30. Liyongo asimuhuli
Akaipeja ya pili
Pandaye isihimili
Na ya pili kapasuwa

Sehemu ya Kati ya Utenzi

- 100 Na tumi wa sulutwan
Akitoka kijumbani
Kaya tumi wa nyumbani
Chakula akimweteya
- 101 Na mamake kwa hakika
Chakula chema kipika

- Asikari humpoka
Xchakula wakailiya
102 Chakula wakimweteya
Asikari huiliya
Siku hiyo kambwambiya
“mamangu nisalimiya”.
- 103 Kanena kwa ushairi
“enenda kamukhubiri
Mama- afanye tayari
Haya nimezokwambiya
104. Kamba “sada nakutuma
Enda kambwambie mama
Afanye mkate mwema
Kati tupa aitiya
105. “ muinga hayalimka
Mle tupa na kupika
Makozi yakaniuka
Nyika hawatajaliya.”
- 106 Sada akabalighisha
Mamake yakamuwasha
Akaufanya wa wishwa
Mkate kampikiya
- 107 Mkate huu sikiya
Pishi mbili hutimiya
Kati tupa akatiya
Liyondo kampekeya

- 108 Asikari kiuona
Ni wishwa wakatrukana
Wa wishwa hula watwana’
Mpekee haya ngiya
- 109 Ule Liyongo chumbani
Kauvunda kwa sirini
Tupa akaona ndnai
Furaha zikamngiya
- 110 Maina tupa akitiya
Kitambaa metatiya
Kwa furaha mno ghaya
Sana kawafurahiya
- 111 Hata usiku kufika
Matezo wakayandika
Kana ada wakaweka
T’asa, pembe, siwa piya
- 112 Na ngoma na nyingi kusi
Kusisalie unasi
Ikawa kama harusi
Watu wakiangaliya
- 113 Wut’e wakakutanika
Mahala pakatandikwa
Na uzuri wakaweka
Deuli na subahiya
- 114 Wakatandika za zari
Na libasi za Hariri

- Wakaimba mashairi
Ngoma na kusi pamoya
- 115 Kula nyimbo zizidipo
Na ngoma zitakatapo
Alikizitinda hapo
Pingu na minyoo piya
- 116 Zilipo kikaza kusi
Alikikata upesi
Hata zikikoma basi
Inukani kawambiya
- 117 Wakiinuka kuteza
Liyongo akatokeza
Khaufu zaliwakaza
Mbiyo zikawapoteya
- 118 Kwa wut'e wakakimbiya
Hapana alosaliya
Liyongo kaitokeya
Mabarani kerejeya
- 119 Sulutwani kawatiya
Askari kumzengeya
Mwane liyongo sikiya
Ili kumuandaliya.
- 120 Wakamuona ndiyani
Wakampeka asikhini
Hata kwenyi sulutwani
Mwane liyongo akaya

- 121 Bawabu kenda darini
 Aketipo sulutwani
 Akaitaka idhini
 Mwana ataka kungiya
- 122 Sulutwani kisikiya
 Mno akafurahiya
 Kwa mwane liyongo kuya
 Akamwambiya “neteya”
- 123 Kapanda naye bawabu
 Kijana kitaajabu
 Nini nimezoharibu
 Ni ipi yangu khatiya
- 124 Kapanda wakaonana
 Pamoya na ule bwana
 Sulytwani akanena
 “ nakuomba yambo moya”
- 125 Kamwambiya “wapendani
 Mimi ni mwako twaani
 Kukhalifu simkini.
 Mimi ni wako raiya
- 126 “kwa baba enda sikhini
 umuulize yakini
 Kimuuwacho ni n’ni
 Nakuomba hili moya
- 127 “Au wewe wakiyuwa

- Nambiya sifanye tuwa
Uwaziri utapowa
T'akuoza bintiya
128 Akamjibu. "sisi
Ya kweli hata kukisi
Ila njoa sasa basi
Khabari t'akuetya".
- 129 Sulutrwani maudhamu
Kijana kamkirimu
Kwa zakula ziko tamu
Kampa na nguo mpiya
130 Ule kijana katoka
Akanenda hata shaka
Kwa babake akifika
Babake kamshashiya

Sehemu ya Mwisho ya Utenzi

- 200 Kuuwa haiwezekani
Kighadhiubika haneni
Huwa zitoni za ndani
Na kuingurumiya
201 Mamakwe kitaajabu
Akinena ni ajabu
Mara hii ameharibu
Ameiza kusikiya

- 202 Kipara siku katiti
 Kaanduka ni maiti
 Wakatambua umati
 Liyongo ameifaya
- 203 Wut'e wakakurubiya
 Mamakwe na watu piya
 Sana wakimwangaliya
 Ni sindano ametiwa
- 204 Ametiwa kitovuni
 Shaba sindano yuwani
 Wakamtia muini
 Akzikwa kwa umoya
- 205 Habari ikaeneya
 Pate ikasikiliya
 Mfalume kitaiwa
 Furaha zikamweneya
- 206 Mwane liyongo yakini
 Mewekwa magodoroni
 Na zakula anuani
 Hula akiinwiya
- 207 Mfslume kipulika
 Liyongo ametoweka
 Nde mui meanguka
 Haya aliazimiya
- 208 Akanena mueteni
 Mwane liyongo yakini

Aye haopa hadharani
 Ni neno t'amwambiya
 209 Akenda aktwaliwa
 Kaya kwa bwana welewa
 Mfalme katongowa
 Khabari akamwambiya
 210 "amekufa baba wako"
 Akaangua kiteko
 Kwake kwamwe sikitiko
 Kabisa halikungiya
 211 Mfalme kamwambiya
 "mbona mwana hukuliya
 Babako alikuyeya
 Kwa anasa zot'e piya?
 212 Ule mwana kwa swahihi
 Kajibu " nimefurahi
 Mentitendea ilahi
 Haya menijaaliya"
 213 Mfalume kabaini
 "kabisa huna imani
 Epuka mwangu matoni
 Na nyumbani nitokeya
 214 " usiketi mui wangu
 Wewe adui ya mngu
 Tena vua nguo zangu
 Vaa yako mazoweya

215 “ kuwa mwana na kigala
Ni adui wa dhalala
Ya babakwe amekula
Damu kwa kuiuliya”

216 Mfalume kamtowa
Nguo zakwe kambvuwa
Na watu akatukiwa
Khabari ikaeneya

217 Kwa jamii ya fijiri
Wakanena si uzuri
Kwa yot’e majimbo piya

218 Yule mwana nikwambiye
Hakwenenda kwa bibiye
Kwa mama liyongo yeye
Galani alikimbiliya

219 Watu akitahayari
Kwa ile yakwe amri
Watu wakimtiriri
Mayuto yakamngiya

220 Kaingiya mayutoni
Katindikia nyumbani
Hata wenzi hawaoni
Hamu imezomngiya

221 Ule mamakwe kijana
Hakumpenda tena
Kimwamba na kunong;ona

- Mno akamtukiya
- 222 Kawa tena hampendi
Kwa chakula hamtundi
Yakamzidi mayondi
Huzuni zikamngiya
- 223 Siku chache kitimiya
Maradhi yakamngiya
Yasiyomuondokeya
Naye kisa kaifiya
- 224 Matanga aliyaweka
Watu wakasikitika
Kwa liyongo kuifiya
- 225 “liyongo silaha yetu
Kwa wut’e khasimu zetu
Alikuwa ngao yetu
Wut’e wakinena haya
- 226 Mui walisikitika
Hakuna wa kutosheka
Kwa liyongo kutoweka
Imeanguka pazi ya
- 227 Sana wakahuzunika
Na matanga wakaweka
Kisa mamake katoka
Kana ada katembeya
- 228 Tumeziya kukhitimu
Hapo ndio wasalamu

Ilahi tatukirimu
Kwa Baraka na afiya
229 Rabi tatusahiliya
Na uzto wa duniya
Tena tatujaaliya
Kuwa njema yetu niya
230 Ya liyongo hukwambiya
Sui alikozaliwa
Pate akitembeleya
Kwa mwana akafiliiya
231 Na kwa mwana ni rasini
Ya shaka iyuweni
Ni mui hapo zamani
Ni mkuu hukwambia
232 Mui waloamirika
Nyumba za mawe hakika
Mayiwe waliyaweka
Na misikiti pamoya.